ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

2016 - 2020

1.	**Mhe. Zubeir Ali Maulid**	**-**	**SPIKA**
2.	**Mhe. Mgeni Hassan Juma**	**-**	**Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake**
3.	**Mhe. Shehe Hamad Mattar**	**-**	**Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni**
4.	**Mhe. Mwanaasha Khamis Juma**	**-**	**Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani**
5.	**Mhe. Balozi Seif Ali Iddi**	**-**	**MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda**
6.	**Mhe. Issa Haji Ussi Gavu**	**-**	**MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka**
7.	**Mhe. Haji Omar Kheri**	**-**	**MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu**
8.	**Mhe. Haroun Ali Suleiman**	**-**	**MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi**

			Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
9.	**Mhe. Mohammed Aboud Mohammed**	**-**	**MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais /Uteuzi wa Rais**
10.	**Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed**	**-**	**MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge**
11.	**Mhe. Mahmoud Thabit Kombo**	**-**	**MBM/Waziri wa Habari, Utalii, na Mambo ya Kale/Jimbo la Kiembesamaki**
12.	**Mhe. Riziki Pembe Juma**	**-**	**MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake**
13.	**Mhe. Balozi Amina Salum Ali**	**-**	**MBM/Waziri wa Biashara, na Viwanda / Uteuzi wa Rais**
14.	**Mhe. Balozi Ali Abeid Karume**	**-**	**MBM/Waziri wa Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo/ Uteuzi wa Rais**
15.	**Mhe. Rashid Ali Juma**	**-**	**MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Amani**

16.	**Mhe. Hamad Rashid Mohamed**	**-**	**MBM/Waziri wa Afya / Uteuzi wa Rais**
17.	**Mhe. Maudline Cyrus Castico**	**-**	**MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais**
18.	**Mhe. Salama Aboud Talib**	**-**	**MBM/Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati / Nafasi za Wanawake**
19.	**Mhe. Sira Ubwa Mamboya**	**-**	**MBM/ Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais**
20.	**Mhe. Juma Ali Khatib**	**-**	**MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Uteuzi wa Rais**
21.	**Mhe. Said Soud Said**	**-**	**MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Uteuzi wa Rais**
22.	**Mhe. Khamis Juma Mwalim**	**-**	**Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe**
23.	**Mhe. Mihayo Juma N'hunga**	**-**	**Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais /Jimbo la Mwera**
24.	**Mhe. Shamata Shaame Khamis**	**-**	**Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi**

				ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Micheweni
25.	**Mhe.**	**Harusi Said Suleiman**	**-**	**Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete**
26.	**Mhe.**	**Mmanga Mjengo Mjawiri**	**-**	**Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani**
27.	**Mhe.**	**Mohamed Ahmada Salum**	**-**	**Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/Jimbo la Malindi**
28.	**Mhe.**	**Chum Kombo Khamis**	**-**	**Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale/ Nafasi za Wanawake**
29.	**Mhe.**	**Shadya Mohamed Suleiman**	**-**	**Naibu Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake**
30.	**Mhe.**	**Lulu Msham Abdalla**	**-**	**Naibu Waziri wa Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo/ Nafasi za Wanawake**
31.	**Mhe.**	**Juma Makungu Juma**	**-**	**Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba , Maji na Nishati / Jimbo la Kijini**
32.	**Mhe.**	**Hassan Khamis Hafidh**	**-**	**Naibu Waziri wa Biashara,**

				na Viwanda /Jimbo la Welezo
33.	**Mhe.**	**Dkt. Makame Ali Ussi**	**-**	**Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Mtopepo**
34.	**Mhe.**	**Abdalla Ali Kombo**	**-**	**Jimbo la Mwanakwerekwe**
35.	**Mhe.**	**Abdalla Maulid Diwani**	**-**	**Jimbo la Jang'ombe**
36.	**Mhe.**	**Ali Khamis Bakar**	**-**	**Jimbo la Tumbe**
37.	**Mhe.**	**Ali Salum Haji**	**-**	**Jimbo la Kwahani**
38.	**Mhe.**	**Ali Suleiman Ali (Shihata)**	**-**	**Jimbo la Kijitoupele**
39.	**Mhe.**	**Ahmada Yahya Abdulwakil**	**-**	**Uteuzi wa Rais**
40.	**Mhe.**	**Ame Haji Ali**	**-**	**Jimbo la Nungwi**
41.	**Mhe.**	**Amina Iddi Mabrouk**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
42.	**Mhe.**	**Asha Abdalla Mussa**	**-**	**Jimbo la Kiwengwa**
43.	**Mhe.**	**Bahati Khamis Kombo**	**-**	**Jimbo la Chambani**
44.	**Mhe.**	**Bihindi Hamad Khamis**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
45.	**Mhe.**	**Hamad Abdalla Rashid**	**-**	**Jimbo la Wawi**
46.	**Mhe.**	**Hamida Abdalla Issa**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
47.	**Mhe.**	**Hamza Hassan Juma**	**-**	**Jimbo la Shaurimoyo**
48.	**Mhe.**	**Hidaya Ali Makame**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
49.	**Mhe.**	**Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa)**	**-**	**Jimbo la Mtoni**
50.	**Mhe.**	**Jaku Hashim Ayoub**	**-**	**Jimbo la Paje**
51.	**Mhe.**	**Khadija Omar Kibano**	**-**	**Jimbo la Mtambwe**

52.	**Mhe.**	**Machano Othman Said**	**-**	**Jimbo la Mfenesini**
53.	**Mhe.**	**Makame Said Juma**	**-**	**Jimbo la Kojani**
54.	**Mhe.**	**Maryam Thani Juma**	**-**	**Jimbo la Gando**
55.	**Mhe.**	**Masoud Abrahman Masoud**	**-**	**Jimbo la Bububu**
56.	**Mhe.**	**Miraji Khamis Mussa**	**-**	**Jimbo la Chumbuni**
57.	**Mhe.**	**Moh'd Mgaza Jecha**	**-**	**Jimbo la Mtambile**
58.	**Mhe.**	**Mohamed Said Mohamed**	**-**	**Jimbo la Mpendae**
59.	**Mhe.**	**Mohammedraza Hassanaali Mohamedali**	**-**	**Jimbo la Uzini**
60.	**Mhe.**	**Mtumwa Peya Yussuf**	**-**	**Jimbo la Bumbwini**
61.	**Mhe.**	**Mtumwa Suleiman Makame**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
62.	**Mhe.**	**Mussa Ali Mussa**	**-**	**Jimbo la Ole**
63.	**Mhe.**	**Mussa Foum Mussa**	**-**	**Jimbo la Kiwani**
64.	**Mhe.**	**Mwanaidi Kassim Mussa**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
65.	**Mhe.**	**Mwantatu Mbaraka Khamis**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
66.	**Mhe.**	**Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini**	**-**	**Jimbo la Dimani**
67.	**Mhe.**	**Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy**	**-**	**Jimbo la Chaani**
68.	**Mhe.**	**Nassor Salim Ali**	**-**	**Jimbo la Kikwajuni**
69.	**Mhe.**	**Omar Seif Abeid**	**-**	**Jimbo la Konde**
70.	**Mhe.**	**Panya Ali Abdalla**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
71.	**Mhe.**	**Rashid Makame Shamsi**	**-**	**Jimbo la Magomeni**
72.	**Mhe.**	**Saada Ramadhan Mwendwa**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
73.	**Mhe.**	**Said Omar Said**	**-**	**Jimbo la Wingwi**

74.	**Mhe.**	**Said Hassan Said**	**-**	**Mwanasheria Mkuu**
75.	**Mhe.**	**Salha Mohamed Mwinjuma**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
76.	**Mhe.**	**Salma Mussa Bilal**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
77.	**Mhe.**	**Shaib Said Ali**	**-**	**Jimbo la Chonga**
78.	**Mhe.**	**Simai Mohammed Said**	**-**	**Jimbo la Tunguu**
79.	**Mhe.**	**Suleiman Makame Ali**	**-**	**Jimbo la Ziwani**
80.	**Mhe.**	**Suleiman Sarahan Said**	**-**	**Jimbo la Chakechake**
81.	**Mhe.**	**Tatu Mohamed Ussi**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
82.	**Mhe.**	**Ussi Yahya Haji**	**-**	**Jimbo la Mkwajuni**
83.	**Mhe.**	**Viwe Khamis Abdalla**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
84.	**Mhe.**	**Wanu Hafidh Ameir**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
85.	**Mhe.**	**Yussuf Hassan Iddi**	**-**	**Jimbo la Fuoni**
86.	**Mhe.**	**Zaina Abdalla Salum**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
87.	**Mhe.**	**Zulfa Mmaka Omar**	**-**	**Nafasi za Wanawake**

Ndg. Raya Issa Msellem **-** **Katibu**

Kikao cha Nne – Tarehe 14 Mei, 2018

(Kikao Kilianza Saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Naibu Spika (Mgeni Hassan Juma) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:

Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha Mezani Hotuba ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mashirika na Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 na Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mawizara ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

Mhe. Hamad Abdalla Rashid (Kny) Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (*PAC*)

Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha Mezani Hotuba ya Kamati ya (PAC) kuhusu Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mashirika na Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanbibar kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 na Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mawizara ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016. Naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 201

Kuwakutanisha Vijana Wanaoishi na Walioambukizwa Virusi vya Ukimwi

Mhe. Omar Seif Abeid – Aliuliza:

Kwa kuwa *ZAPHA+* kwa kushirikiana na vijana wa Wilaya ya Micheweni wameanzisha Club maalum ambayo lengo lake ni kuwakutanisha vijana na kuwatambua vijana wanaoishi na walioambukizwa virusi vya ukimwi ili vijana hao waweze kuhudhuria kliniki na kupata ushauri na kwa sababu kwa sasa kasi ya maambukizi hayo yapo zaidi kwa rika la vijana wadogo ambao kama hatua za makusudi hazitochukuliwa vijana wengi wataathirika.

Je, Serikali ina mpango ngani wa kuzisaidia Jumuiya kama hizo ambazo zimejitolea kwa makusudi dhidi ya kuhamasisha vijana kwenye mapambano na maambukizo ya virusi vya ukimwi.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Alijibu:

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Omar Seif Abeid swali lake Nam. 201 kama ifutavyo, naomba kutanguliza maelezo yafuatayo:-

Mhe. Naibu Spika, Serikali inathamini asasi zisizo za Kiserikali kama *ZAPHA+* katika kusaidia mapambano dhidi ya UKUMWI. Ni kweli katika miaka ya hivi karibuni taarifa zinaonesha kwamba maambukizi mapya ya VVU yanawapata zaidi vijana wenye umri baina ya miaka 15 hadi 24. Hivyo basi kuanzishwa kwa klabu maalum Wilaya ya Micheweni na *ZAPHA+* kwa lengo la kuwasaidia vijana wanaoishi na VVU ni jambo la kuwapongeza na kupigiwa mfano.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo kwa ruhusa yako sasa naomba kumjibu Mhe. Omar Seif Abeid swali lake Nam. 201 kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, Serikali kupitia Tume ya UKIMWI na Wizara ya Afya imekuwa karibu sana na Jumuiya kama *ZAPHA+* katika mapambano dhidi ya UKIMWI. Serikali inaendelea kuzijengea uwezo katika maeneo mbali mbali ikiwemo kuwapatia elimu ya ujasiriamali, fedha kwa miradi midogo midogo kupitia kwa wahisani wetu wa maendeleo, elimu ya ushauri nasaha, matumizi sahihi ya dawa za kupunguza makali ya VVU, misaada ya chakula pale fursa zinapojitokeza na kuwajengea uwezo wa kuweza kujitafutia rasilimali fedha kupitia miradi mbali mbali ya maendeleo. Nakushukuru Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipatia fursa ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali dogo la nyongeza. Kwanza nachukua nafasi hii kuipongeza serikali kwa majibu mazuri yenye mwelekeo kwa ajili ya kupambana na maradhi haya ya ukimwi ambapo Mhe. Waziri amekiri kwamba rika linaloathirika sasa ni la vijana kati ya miaka 15 hadi 24, lakini nilikuwa napenda tu nijuwe kwamba kwa kuwa hawa wanaklabu wa Wilaya ya Micheweni wamejitolea na ukitilia maanani uwezo wao bado ni mdogo.

(a) Je Wizara ina mpango gani wa kuwasaidia kama *Club* ukiachilia mbali *ZAPHA+* ili waweze kujiendeleza.

(b) Ni nini wito wako kwa serikali au kwa wananchi kwa Zanzibar yote kuanzisha *Club* kama hizi ili kutoa nasaha na elimu kwa vijana kuhusiana na maambukizi mapya ya VVU. Ahsante sana Mheshimiwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Alijibu:

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Omar Seif Abeir swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, kama ambavyo nimejibu katika jibu langu la msingi, serikali inafanya kazi kwa karibu zaidi na imeanza kuwapongeza wenzetu wa Micheweni kwa kuanzisha Asasi hii, tutalichukua hili na tutakwenda Micheweni tutashirikiana nao kama Wizara na Serikali tutajua namna gani ya kuweza kuwasaidia hasa kwa mujibu wa hitaji lao na mazingira yaliyokuwepo katika Wilaya ya Micheweni.

(b) Mhe. Naibu Spika, wito wangu kwa Serikali na Asasi zote za kiraia mapambano dhidi ya Ukimwi ni jambo letu sote kama ambavyo tumelizungumza katika uwasilishaji wa Bajeti yetu ni sasa serikali tunawajibu wa kuweka mkazo katika hili kundi kubwa ambalo kwa sasa limekuwa likipata maambukizi makubwa ya VVU katika umri wa kuanzia miaka 15 mpaka 25 ni kweli jambo hili ni vyema familia kwa ujumla katika ngazi zote za serikali ni vyema tukashirikiana kwa pamoja na serikali kuu tukaongeza elimu ya kutosha na tahadhari hasa kwa vijana wetu kuepukana na vishawishi vidogo vidogo visivyokuwa na tija wala sababu za msingi ambazo zinapelekea wao kujiingiza katika makundi yasiyokuwa na sababu za msingi. Nakushukuru Mhe. Naibu Spika.

Nam. 233

Kuanzisha Mkoa wa Kiserikali kwa Ajili ya Wilaya ya Magharibi "A" na "B"

Mhe. Machano Othman Said – Aliuliza:

Wilaya ya Magharibi "A" na "B" zina wakaazi wasiopungua 350,000 kwa mujibu wa sensa ya 2012, idadi ambayo inaongezeka kila siku kutokana na kiwango cha uzazi na uhamiaji usio na mipaka hali ambayo imesababisha Wilaya hizo kukabiliwa na matatizo mengi ikiwemo tatizo sugu la maji safi na salama, uchache wa madarasa, mafuriko ya mara kwa mara, kutokuwa na hospitali za Wilaya na miundo mbinu mibovu ya barabara.

(a) Je, Serikali haioni kwamba wakati umefika sasa wa kuanzisha Mkoa wa Kiserikali kama kilivyoamua Chama cha Mapinduzi mwaka 2012.

(b) Ni lini Serikali itaweka mkakati maalum wa kuondoa kero hizo za wananchi wa Wilaya hizo.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Machano Othman Said swali lake Nam. 233 lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, ni kweli kuwa kukuwa kwa kasi ya ongezeko la idadi ya watu katika Wilaya za Magharibi 'A' na 'B' linachangia upatikanaji hafifu wa huduma za kijamii hususan za elimu, maji, miundombinu ya barabara na huduma nyenginezo. Ongezeko hilo la watu haliendani sambamba na ukuwaji wa uwekezaji katika miundombinu ya

huduma mbali mbali za kijamii. Hali hii inapelekea miundombinu iliopo kushindwa kukidhi mahitaji halisi ya wananchi waliopo katika Wilaya hizo.
Mhe. Naibu Spika, Serikali kwa kulitambua hilo, inaendelea na hatua zake za kuimarisha upatikanaji wa huduma za jamii kwa kuzingatia mipango yake ya katika mipaka ya utawala iliyopo.

(b) Mhe. Naibu Spika, hata hivyo, kama Mhe. Mwakilishi anahisi kuanzishwa kwa eneo jipya la utawala (Mamlaka ya Mkoa) linaweza kuchochea kuharakisha upatikanaji wa huduma katika Wilaya hizo, nataka nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba Serikali imeupokea ushauri huo na itaufanyia kazi.

Mhe. Naibu Spika, hakuna mkakati mahsusi ambao Serikali imeuweka kwa ajili ya kuondoa kero za wananchi wa Wilaya za Magharibi 'A' na 'B', badala yake Serikali inaendelea kutatua kero za Wilaya hizi na Wilaya nyenginezo kwa kuzingatia Dira ya 2020 na Mipango Mikuu ya Kitaifa (Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini – Mkuza na Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015/2020.

Mhe. Naibu Spika, katika kutekeleza mikakati hiyo ya Kitaifa ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaimarisha huduma za kijamii katika Wilaya zote za Unguja na Pemba. Katika sekta ya elimu, Serikali kwa kushirikiana na washirika wa maendeleo inaendelea kukamilisha ujenzi wa skuli nne (4) mpya na za kisasa katika Wilaya ya Magharibi "B" maeneo ya Fuoni na Kwarara ambazo zitapunguza kwa kiasi kikubwa uhaba wa madarasa na kuwezesha kuwa na mazingira bora ya kusomea. Aidha, katika mwaka wa fedha wa 2018/2019 Serikali imepanga kukamilisha ujenzi wa madarasa ya skuli za Mbuzini na Abdalla Sharia zilioko katika Wilaya za Magharibi 'A' na "B".

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa afya, Serikali inaendelea kuimarisha upatikanaji wa dawa, usambazaji wa dawa, vifaa tiba, dawa za uchunguzi wa maradhi na *"reagents"* katika vituo vyote vya afya vinavyomilikiwa na Serikali vikiwemo vituo 16 vilioko katika Wilaya za Magharibi "A" na "B". Hatua za kuimarisha miundombinu ya barabara nazo zinaendelea kwa ujenzi wa barabara ya Kwamabata hadi Kijitoupele kupitia Nyarugusu na ile Pangawe hadi Fuoni Mambosasa kwa kiwango cha lami.

Mhe. Machano Othman Said : Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa Mkoa wa Mjini/Magharib sasa Serikali inakadiriwa kuwa na watu wasiopungua laki 7 na kwa kuwa mkoa huo wa Mjini/Magharib una majimbo ya Uchaguzi 22, mjini 9 na magharib (A) na (B) 13.

(a) Je serikali haoni kwamba wakati umefika sasa wa kuanzisha mkowa mpya wa kiserikali. Pamoja na nia nzuri ya serikali lakini wakiangalia na idadi ya watu na mahitaji yao hawaoni kwamba Magharib inastahiki ni mkowa wa kiserikali kuwa Mkowa wa kiserikali kama ilivyo Chama cha Mapinduzi

(b) Wilaya Magharib (A) ambayo ni mpya zaidi haina hata kituo cha kununulia umeme wilaya hiyo haijapangiwa hata barabara moja kutengenezwa na Wilaya hiyo ndiyo

ambayo inatoa maji kwa mji wa Zanzibar karibuni kwa asilimia 70 mpaka 80 kwa nini serikali isione kwamba kuna haja kuimarisha huduma hizo kwa kupitia mkowa mpya wa kiserikali.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Machano Othman Said swali lake la nyongeza lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, ni kweli Mhe. Mwakilishi atakumbuka katika jibu langu la msingi nimesema kwamba ushauri ambao Mhe. Mwakilishi ameutoa ni ushauri ambao tumesema tutauchukua na tutaufanyia kazi tuone kwamba jambo hili linafanikiwa kwa mujibu ambavyo itaonekana hali inaruhusu katika kutekeleza jambo hilo. Kwa hiyo, naomba nirejee kusema Mheshmiwa Mwakilishi ushauri huo wakuweza kuona kwamba tuna mkoa mwengine kama vile Kichama ni jambo la ushauri na tumesema tumelichukuwa.

(b) Mhe. Naibu Spika, ni kweli katika Wilaya ya Magharibi (A) katika miundombinu hizo ambazo Mhe. Mwakilishi amezisema ni kweli bado hadi sasa hivi hakujawa na utelekezaji ambao uko vizuri. Naomba niendelee kumpa matumaini Mheshimiwa Mwakilishi kwamba mikakati ya kuimarisha Magharib (A) kama ambavyo tumeweza kumjibu katika maswali mbali mbali basi naomba nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi tumeomba kwamba umuhimu upo wa kuwepo na kituo cha kuuzia umeme, lakini vile vile na miundombinu ya barabara naomba nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba malalamiko hayo au changamoto hizo serikali imezipokea na itaendelea kuzifanyia kazi siku hadi siku kuona kwamba nayo imekuwa kama Wilaya nyengine. Ahsante.

Mhe. Salma Mussa Bilal: Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa hii ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Waziri, ni lini serikali itakimaliza Kituo cha Afya cha Mbuzini ambacho kimejengwa kwa nguvu za wananchi na sasa hivi ni cha muda mrefu ambacho kitawapunguzia usumbufu wananchi hao na hasa ukizingatia kwamba kituo hicho kimezungukwa na maeneo mbali mbali ambayo yatafaidika na kituo hicho.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Salma Mussa Bilal swali lake la nyongeza lenye kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, ni kwamba naomba kutowa maelezo mafupi azma ya serikali katika kujenga vituo vya Afya vingi katika meoneo mbali mbali hapa nchini dhamira yake ni kupeleka huduma kwa wananchi na kutatuwa kero zao kwa mujibu ambavyo zinatokea katika maeneo husika. Hivyo nimwambie Mhe. Mwakilishi ujenzi wa kituo hicho umejengwa kutoka na dhamira ile ile ya kuondoa kero za wananchi katika maeneo hayo hivyo naomba kwa kuwa tumeanza na

Ugatuzi naomba tupe muda kidogo ili kusudi tupokee ugatuzi wetu huo na hatimae tufike tuone ni nmna gani kituo hicho tunaweza tukakifanyia kazi kwa haraka zaidi ili kiendelee na dhamira ile ile ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Ali Suleiman Ali : Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Machano Othman Said kwa swali lake zuri na la msingi kabisa katika kuimarisha huduma za jamii katika nchi yetu, lakini pamoja na hayo Mheshimiwa naomba kuuliza swali lifuatalo:

Kwa kuwa Mkowa wa Mjini/Magharib ni mkowa mama kwa bahati katika muundo mpya tuna Manispaa tatu (3) Manispaa ya Majini, Manispaa ya Magharib (A) na Manispaa ya Magharib (B) kwa kuwa hayo yote yapo lakini utendaji umekuwa mgumu kutokana na mazingira mbali mbali ya hali halisi ya miundombinu swali langu lipo hapa, pamoja na hayo yote Mkoa wa Mjini/Magharib ni mkoa wa mwisho kuwa na ofisi ambayo haitambuliki kiutaratibu wa ofisi na katika kiwanja chetu cha Amani kimezungushwa mabati zaidi ya mwaka wa sita sasa hivi au wa tatu mabati yanaibiwa yanawekwa mengine hivyo Mhe. Waziri atueleze lini ujenzi wa ofisi ya Mkoa wa Mjini/Magharib utaanza kujengwa ili tuwe na hadhi ya mkoa hasa tulingalisha kwamba Makao Makuu ya Serikali yapo mkoa huu wa mjini magharib.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Ali Suleiman Ali swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, ni kweli katika ofisi ya Mkuu wa Mkoa anayoitumia sasa hivi ni kwamba haiendani na hali halisi ya mazingira tuliyokuwa nayo katika kutoa huduma kwa wananchi wetu hususan katika Mkoa huu ambao umekuwa na ungezeko kubwa la wananchi na unahitajika huduma nyingi. kwa hivyo, kutokana na hali hiyo serikali imedhamiria kulijenga eneo lile ili kusudi kuwa na ofisi ya kisasa ili kusudi kuweza kuondoa tatizo hilo ambalo Mhe. Mwakilishi amekuwa akilizungumzia na sisi kama ofisi ya Rais Tawala za mikoa Serikali za mitaa jambo hili tumeliona, tumeliona na umuhimu upo na tunaendelea kufanya jitahada mbali mbali pale ambapo hali itaruhusu upatikanaji wa fedha, naomba nimwambie Mhe. Mwakilishi na sisi jambo hili lilnatukera na tutahakikisha kwamba kazi hiyo inafanyka *soon* tu baada ya kupatikanaji wa fedha katika eneo lile basi ofisi iweze kuonekana kwa muonekano wa kisasa zaidi.

Nam. 88

Magonjwa Ya Mwani Yaliyojitokeza Katika Kijiji Cha Kitogani

Mhe. Bahati Khamis Kombo – Aliuliza:

Hivi karibuni kumejitokeza wakulima wa Mwani katika kijiji cha Kitogani kulalalamikia magonjwa yaliyojitokeza katika zao hilo na kuwarudisha nyuma kwa Kilimo hicho.

(a) Je, Wizara imeshakwenda kuona tatizo hili.

(b) Je, na kama tayari Serikali imechukuwa jitihada gani kuona kuwa wanawasaidia wananchi hao.

(c) Je, Serikali imefanya utafiti katika eneo hilo.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo Maliasili, Mifugo na Uvuvi – Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi suali lake lenye vifungu (a) (b) na (c) kama ifuatavyo:-

a. Mhe. Spika, Wizara yangu tayari imetembelea maeneo yote yaliyoathirika na magonjwa likiwemo la Kitogani. Aidha, maradhi hayo husababishwa na mabadiliko ya tabia nchi (jua kali) na hatimae mwani haukuwi na kustawi vizuri.
b. Mhe. Naibu Spika, hivi sasa Wizara yangu inaendelea na tafiti mbali mbali ikiwa ni pamoja na kuwashajihisha wakulima wa mwani kupanda mwani wao katika kina kirefu cha maji (sio chini ya mita 2). Aidha, katika tafiti zetu mfumo wa kupanda mwani unaofungwa na nyavu za uvuvi katika kina kirefu cha maji zinaendelea kufanywa na kuona kwamba zinaleta tija ili baadae elimu hiyo itolewe kwa wakulima wa mwani.

Mhe. Spika, naomba kulieleza Baraza lako tukufu kwamba utafiti ni jambo endelevu na wizara yangu inaendelea na utafiti siku zote, na utafiti wetu kwa kweli unalenga ama kuondoa zile *recommendation* ziliopo sasa hivi au kuongeza taaluma katika ile *recommendation* iliyopo sasa hivi au kufanya *correction* au kuthibitisha ile iliyopo sasa hivi.

Mhe. Bahati Khamis Kombo: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika kwanza kabisa nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri lakini pia naomba kumuliza suala moja la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kama alivyoeleza katika jibu lake mama kwamba wanaendelea kufanya tafiti pamoja na kuwashaijisha wananchi kupanda mwani katika kina kirefu cha maji. Je, kwa nini kabla ya kupanda wasiweze kuwashajiisha na wakawapa maelekezo mazuri ya kupanda mwani na badala yake sasa hivi wanaendelea kupata hasara ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi Bi Bahati swali lake la nyongeza kama ifuatavyo: -

Hatua ya kuwaeleza wakulima wetu wa Mwani walime kina kirefu iyo ipo muda mrefu, na hivi sasa tutakana tuithibitishe kwa tafiti maalum ambayo itabidi tuwaeleze uhakika wa mambo, kwa

sababu hatutaki kukurupuka tu kufanya maelezo ambayo pengine yanaweza yakapotosha zaidi. Kwa hivyo, tunasisitiza kufanya utafiti na kama nilivyoeleza hapo awali kwamba tunaendelea kufanya ufati ili kuhakikisha kila jambo muhimu la mwani linalohitajika kufanyika ili upatikane faida zaidi basi linafanyika kwa taaluma hiyo.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwanza nikiri kwamba nampongeza sana Mhe. waziri kwa kukiri kwamba mwani una matatizo kutokana na mabadiliko ya tabia nchi ni kweli Mhe Naibu Spika, lakini amesema kwamba wakulima wanashauriwa walime mwani kwenye kina kirefu cha maji. Mhe. Naibu Spika, wanahitaji vyombo vya kuweza kufika kule kwenda kupanda mwani huo. Je, huoni kwamba wakulima na watasumbuka hapo na pia mwani utaadimika Zanzibar. Lakini pia vile vile ni lini Wizara yako imejipanga kuhakikisha wakulima wa mwani wamepatiwa vyombo vya uhakika vyenye mashine ili kufika huko kwenye kina kirefu cha maji?.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi naomba kumjibu Mhe. Suleiman Makame Ali swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kina kirefu tulichokiweka cha mita mbili maji yanapotoka yanakua sio kirefu sana sasa tunawashauri wanapanda maji wakati yametoka halafu baadae tena maji yakijaa wanakuwa kwenye kina cha mita mbili, lakini hata hivyo hata kwenye nyavu hizi pia wanapanda mwani na wanapata vizuri sana huko maji marefu vile vile. Kwa hivyo, nasisitiza kwamba utafiti zaidi unatakiwa ufanyike ili tuweze kupata ile *recommendation* inayotakiwa(*Makofi*).

UTARATIBU

Mhe. Suleiman Makame Ali: Waziri au Naibu Waziri atajibu swali kwa ukamilifu kabisa Mhe. Naibu Spika, nilimuuliza kwamba Wizara yako ina mpango gani kwa sababu Mhe. Naibu Spika pima mbili za maji ni lazima papatikane chombo kwa sababu mtu ni pima moja pima mbili inaongezeka juu, sasa Mhe. Naibu Waziri hakunijibu Wizara yake ina mpango gani wa kuwapatia vyombo hivyo, kwa sababu unakuwa hadi pima sita mpaka saba Mhe. Naibu Spika nilitaka nijue Mhe. Naibu Waziri kwa niaba ya wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Naibu Waziri majibu sahihi Mjumbe anataka.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika kwa ruhsa yako naomba kumjibu Mhe. Suleiman Makame Ali swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Tumesema mita mbili kina cha mita mbili lakini wapande wakati maji yametoka kinakuwa sio mita mbili, lakini hata hivyo tumesema tunafanya utafiti tukiona kuna haja ya kuwapatia vifaa vile vinavyohitajika kwenda kina kirefu basi tutafanya hivyo.

Mhe. Waziri wa Afya (Kny: Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi) Mhe. Naibu Spika, kwa idhini ya Waziri wa Kilimo, Maliasili na Uvuvi, naomba kuongezea majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri kama ifuatavyo:-

Kama munakumbuka Waheshimiwa Wawakilishi, Rais ameshatoa maamuzi kuhakikisha kabisa wakulima wa mwani wapatiwe viboti vidogo vidogo vya kuweza kwenda kuchukua. Serikali imechukua juhudi ya kutafuta boti hizo kwa kupitia wafanyabiashara binafsi na kazi hiyo inaendelea na waziri anaishughulikia na mimi naamini kabisa katika muda mfupi ujao agizo la Rais la kupatiwa viboti kwa wakulima hao wa mwani vitapatikana ahsante sana Mhe.

Mhe. Waziri wa Kilimo Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Naibu Spika, nimesimama mimi Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kwanza kumpongeza Mhe. Naibu Waziri wangu wa Kilimo Maliasili, Mifugo na Uvuvi kwa kujibu maswali kwa ufasaha katika fani hii ya kilimo. Aidha si kwa umuhimu wake nimpongeze Mhe, aliyekuwa Waziri wa Kilimo, Mifugo, Maliasili Mifugo na Uvuvi kwa msaada wa ufafanuzi wa swali la nyongeza bado halikujibu hoja ya kanuni ya Mhe. Suleiman Ali Makame ambaye alitoa Kanuni ya 37 kwa kutaka jibu la ufasaha zaidi juu ya mpango wa mwani ambao wengi ni wanawake na hatua ya kuweza kupanda mwani katika kina kirefu ukizingatia maji ya bahari ya kina kirefu kwa wanawake ni jambo ambalo linahitaji uwezeshaji zaidi.

Mhe. Naibu Spika, naomba kulijulisha baraza lako tukufu kwamba mpango wa wizara yangu ni kuhakikisha utafiti kwa maji yanapotoka na yanapojaa,ili kuwezesha mwani kupandwa ndani ya kina cha maji cha mita mbili kwa utaalam uliopo wa kawaida na ule wa kutumia kamba za kuzuia kwa kutumia nyavu.

Mhe. Naibu Spika kwa mujibu wa suala la Mhe. Mwakilishi utafiti tunaoendelea nao ni mpango wa muda mrefu sasa (muda mfupi) ili mpango wa muda wa kati ni kutoa taaluma ya tija ya kilimo cha mwani kutokana na matokeo ya utafiti (*recommendation*) ambapo njia yenye uzalishaji bora zaidi utawafikiwa na utafiti. Upande wa muda mrefu ni kuwawezesha wakulima wetu kama jukumu la serikali kuwafanya wananchi wake wajiajiri zaidi kwa kilimo cha mwani.

Mhe. Naibu Spika, majibu ya Mheshimiwa aliyekuwa Waziri wa Kilimo Maliasili Mifugo na Uvuvi aliyepita la kuwapatia vidau na boti wakulima wa mwani kulima kina kirefu cha maji (mita mbili) sio mpango uliopo hivi sasa ulipangwa kutekelezwa huko nyuma na wananchi wasiuchukue kuwa ni maamuzi ya wizara yaliyotolewa na wizara yangu ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi katika baraza lako kuwasilisha jibu kwa niaba ya wananchi waliwateuwa Waheshimiwa Wawakilishi mpango huo unaweza kuwa kutokana na majibu yake ya kuyafikiria kitafiti ahsante Mhe. Naibu Spika naomba kutoa jibu.

Mhe. Makame Said Juma: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza kwa Mhe. Waziri pamoja na majibu yake mazuri lakini naamini badi hawajafanya utafiti wa kutosha katika bahari inaonoshe bado niwageni lakini ningeomba tu waongezee safari za kwenda tena kwa sababu wajuwe wazi kama ukilima wa mwani sana ni wanawake na hapa wanasema kama upandwe maji mengi. Mhe. Niabu Spika, kwa kweli ningeomba Mhe. Waziri ajipange vizuri kwanza lakini je, niulize wakati watakapokwenda maji makubwa kwenda

kuupanda mwani lakini wajuwe wazi je washaona kama mwani ni chakula cha samaki na mara nyingi sana unapopandwa maji mengi huliwa na samaki? (*Makofi*)

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako na kwa idhini ya Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili na uvuvi naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi Makame Said Juma swali lake kama ifuatavyo:-

Kwanza amesema utafiti haujatosha, utafiti hautoshi Mheshimiwa, siku zote unafanya utafiti na nimeeleza pale mwanzo kwamba lengo la utafiti ku-*replace* ile *recommendation* iliyopo yaani ni kuondoa ile *recommendation* ambayo ipo au inawezekana ukaongeza taaluma kwenye ile iyopo au ukafanya *correction* kwenye iliyopo au uka-*confirm* ile iliyopo ndio inavyokwenda hivyo ndivyo nilivyosema. Kwa hivyo, utafiti ni suala endelevu na tutaendelea na sisi tulivyoingia pale suala la mwanzo tunalifanya kwa kila sehemu ya kiwanda cha kilimo tumejipanga kufanya marekebisho, yale yaliyokuwa mazuri tutayaendelea nayo kwa uzuri zaidi na yale ambayo kwa kweli yatakuwa yana matatizo basi tutayafanyia marekebisho.

Kwamba ni kina mama ambao ndio wanaopanda mwani ndio kweli kwa kweli ndio wanaojishughulisha ni kweli kina mama ndio wanaopanda mwani na tunawahamasisha kina mama wazidi kupanda mwani na hata kina baba washiriki kupanda mwani hakuna anekatazwa hili ni jambo la uchumi kwa hivyo, watu wote wanakaribishwa vijana, wazee, watoto, wote wenye uwezo wa kupanda mwani basi washiriki katika kupanda mwani. Hivyo nanisitiza kwamba Mhe. Makame ajue kwamba sisi tunafanya utafiti na tunaendelea kufanya utafiti na tikigundua kuna mbegu itafaa hayo maji unayosema maji kidogo kwa ajili ya akina mama basi tutaileta mbegu hiyo tuwape kina mama wapande hayo maji kidogo.

Lakini suala la tabia nchi tunasema kwamba maji unaathirika sana kwa maji haya yanayotoka mvua inapokuwa kubwa yakiingia kwenye bahari mwanzo mwanzo pale yanaathiri sana mwani na kwa mwani ule mnene mnene ule unaitwa *cotton* unaweza ukapata maradhi yanaitwa ice ice maradhi yale meupe, unakuwa mweupe mweupe na hii *cotton* inakua ndio ambayo tunaitegemea kwa hivyo, nasisitiza tena kwamba bado utafiti unahitajika ili tuweze kupata mwani utakaohimili matatizo haya.

Nam. 3
Kuanzishwa Mfumo Wa Kuwachuja Wanafunzi Katika Skuli Za Binafsi

Mhe. Shehe Hamad Mattar – Aliuliza:

Kwa kuwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imetoa fursa kwa mtu yeyote awe mzalendo au mgeni kuwekeza katika sekta ya elimu hapa Zanzibar.

Na kwa kuwa fursa hiyo imepokelewa vyema kwa kuanzishwa skuli na vyuo mbali mbali vya kitaifa na kimataifa. Hata hivyo, kuna baadhi ya wawekezaji wa skuli binafsi wameanzisha na kuendeleza mfumo ambao unasumbua wanafunzi na wazazi na ni kinyume cha mikataba yao, kwa kuwachuja wanafunzi wa kidato cha nne ambaye atashuka kidogo alama (*marks*)

walizoweka, hutakiwa kuendelea kusoma skuli ile ile, lakini mtihani wa mwisho wa Taifa akafanye skuli nyengine wanayoijua wao na kwa malipo mengine.
(a) Je, Wizara yako inalijua suala hilo.

(b) Je, Serikali inakubaliana na mfumo huo kutumika kwa wananchi wake na unakubalika katika sera za elimu hapa Zanzibar.

(c) Je, Serikali itachukua hatua gani kwa skuli zote zenye kutekeleza mfumo huo ambao tayari wameshaueleza kwa wanafunzi na wazazi wao, ili kuwaondolea usumbufu mkubwa watoto wetu hapa nchini.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali – Alijibu:

Mhe. Spika**,** kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Elimu, na Mafunzo ya Amali naomba kumjibu Mhe. Shehe Hamad Mattar swali lake Nam. 3 lenye vifungu (a), (b) na (c).kwanza naomba kutoa maelezo ya utangulizi kama hivi ifuatavyo:-

Skuli za sekta binafsi zimeanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu namba 6 ya mwaka 1982. Skuli hizo zimechangia katika kuongeza upatikanaji wa nafasi za elimu na kuimarisha ubora wa elimu katika nchi yetu. Pamoja na mchango wa sekta binafsi, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ndio yenye mamlaka kamili ya usimamizi na utoaji wa miongozo ya uendeshaji wa skuli zote zikiwemo za sekta binafsi. Skuli zinazowachuja wanafunzi wa kidato cha nne na kuwalazimisha baadhi yao kufanya Mtihani wa Taifa wa kidato cha nne katika kituo chengine au skuli nyengine ni kosa kisheria.

Baada ya maelezo hayo ya utangulizi naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi kama hivi vifuatavyo:

(a) Wizara yangu haijapokea taarifa rasmi ya skuli binafsi yenye mtindo wa kuwachuja wanafunzi wa kidato cha nne wasiofikia kiwango cha ufaulu kilichowekwa na skuli na kuwalazimisha wanafunzi kuendelea na masomo na baadae wafanye Mtihani wa Taifa wa kidato cha nne katika skuli nyengine au katika kituo chengine.

(b) Serikali haikubaliani na utaratibu huo ambao ni kinyume na tataribu na sheria ya elimu.
(c) Pindipo kama kuna skuli binafsi zinayofanya vitendo hivyo watambue kuwa ni kosa na hivyo ninaziagiza ziwache mtindo huo mara moja na kama zitagundulika zinafanya hivyo zitachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria. Ninawashauri wazazi na wanafunzi wa skuli binafsi watakaolazimishwa kusoma katika skuli binafsi na wanaposhindwa mtihani wa skuli wanalazimishwa kufanya Mtihani wa Taifa wa Kidato cha nne katika skuli nyengine watoe taarifa rasmi kwa Wizara ili iweze kulifuatilia suala hilo na kuchukua hatua za kisheria.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Mhe. Naibu Spika nashkuru kwa kunipa fursa hii niulize suala la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwanza nimshukuru sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu mazuri na yenye ukweli kabisa lakini naomba uniruhusu kwa kuwa jambo hili linakera hata Serikali ya Jamhuri ya Muungano liko

linaendelea na Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. John Pombe Magufuli alilikemea sana. Nina nukuu ndogo naomba nitowe. Alipokuwa Chuo Kikuu cha Mkwawa shule za *private* wanachuja wale vilaza wanaachwa na kuchukua wale *cream* ili waongoze. Serikali haiwezi ikafanya mambo ya kipuuzi hivi hawana interest ya kila Mtanzania, *interest* yao ni pesa na kutengeneza jina.

Mhe. Naibu Spika, tumemsikia Rais wetu wa Jamhuri wa ya Muungano wa Tanzania akikemea jambo kama hili na kwa Zanzibar ziko shughuli kama hizi. Kama hajapokea taarifa basi kuanzia sasa ndio nampa taarifa rasmi ajuwe kwamba hili linafanyika. Ushahidi upo naomba niitaje ni Skuli ya International Al Haramain tayari wanafanya zoezi kama hilo. Wanafunzi ambao wamechujwa wamepangiwa Skuli ya Suncity ambayo iko Darajani pale Mkunazini, tayari watu hawa wanapangiwa kufanya hivyo.

Je, serikali iko tayari kulikemea suala hili na kufuatilia shule zote ambazo ni za *private* ambazo zina mtindo huu na kuona kwamba wanarejea skuli zao za zamani, na gharama zile ambazo wameingizwa wazazi wanarejeshewa wenyewe. Je, serikali iko tayari kwa kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Naibu Spika, ni kwamba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali itakapopata taarifa rasmi itazichukulia hatua skuli hizo.

Mhe. Naibu Spika, niseme kwamba tunawaomba kama tulivyotanguliza kusema kwamba wazazi na hata wanafunzi wenyewe ambao watakuwa wanafanyiwa hivyo, basi watowe taarifa wizarani na wizara itachukua hatua. Lakini hata hivyo, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali tunafanyakazi wakati mwengine kwa taarifa za fununu ili baadae kuthibitisha. Kwa hivyo, suala hili tutalifuatilia ili kuliona ukweli wake. Endapo tutagundua kuna ukweli fulani basi taratibu na hatua za kisheria zitatumika. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa fursa hii, pia nimsifu Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Lakini nimwambia Mhe. Naibu Waziri kwamba lisemwalo lipo na kama halipo lipo nyuma laja.

Mhe. Naibu Spika, kulikuwa kuna *professor* mmoja alikuwa akiwahutumia watu alisema Mwenyezi Mungu hayupo. Lakini kuna mwendawazimu mmoja akamuambia hujamuona wewe lakini yupo. Kwa hivyo, nataka nimwambie Mhe. Naibu Waziri, kwamba hilo lisemwalo lipo na kama halipo laja.

Sasa nimuulize Mhe. Naibu Waziri kwamba je, umeshafanya vikao na wazazi wa mashule ya binafsi mara ngapi katika Zanzibar?

Je, ukikuta suala kama hilo lipo ili kujirekebisha kwa ile shule, ni adhabu gani ambayo watapatiwa shule ile?

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza Mhe. Mjumbe kama ifuatavyo. Mhe. Naibu Spika. Serikali lazima tulifanyie utafiti, lazima tulipatie ushahidi wake.

Kwa hivyo, kwetu sisi tutaliendeleza kama tulivyotangulia kusema, tutalichunguza kama ni la ukweli taratibu zitachuliku. Endapo litagunduliwa bila shaka kuna hatua au maelekezo mbali mbali, tunaweza kuwaonya na wakirejea tena tutachukua hatua kali zaidi, inaweza kuwa hata hatua ya kufunga skuli kama atakaidi, lakini tutakwenda hatua kwa hatua kwa sababu lengo ni kukumbushana na kuelimisha. Kwa hivyo, tutaendelea kukumbushana.

Mhe. Naibu Spika, tumeshawahi kufanya vikao. Mimi binafsi yangu nimeshafanya vikao, kwa mfano na wamiliki, wakurugenzi na wazazi wa skuli binafsi za skuli za Pemba nimeshafanya, nimeshafanya hata na Unguja pia. Ahsante sana.

Nam. 38

Kukamilika Kwa Ujenzi wa Vyuo Vya Mafunzo ya Amali Vya Daya Mtambwe na Makunduchi

Mhe. Ali Khamis Bakar – Aliuliza:-

Naipongeza wizara yako kwa kutoa elimu ya mafunzo ya amali kwa wanafunzi kulingana na mahitaji ya soko la ajira, ili kuwawezesha vijana kitaaluma ili waweze kujiajiri. Hata hivyo, ujenzi wa chuo cha amali cha Daya Mtambwe na Makunduchi hauridhishi hata kidogo na muda wa ujenzi huo unamalizika.

(a) Je, ni lini ujenzi huo utakamilika.

(b) Je, Wizara ina mpango gani wa kuupitia mkataba wake na ushauri wa mshauri elekezi wa miradi hiyo kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwalimu Mkuu ili kuchukuwa hatua stahiki.

(c) Je, Wizara ina utaratibu gani wa kuwa karibu na washauri elekezi wa miradi yake ya ujenzi na kuhakikisha kuwa wanatekeleza majukumu yao kwa maslahi ya Wizara kama ilivyo katika mkataba.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam 38 lenye vifungu (a), (b) na (c).

Kwanza naomba kutoa maelezo ya utangulizi kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kuwa ujenzi wa Vituo vya Mafunzo ya Amali huko Daya Mtambwe Pemba na Makunduchi Unguja hauridhishi. Kuchelewa kwa ujenzi wa vituo hivyo umechangiwa na mambo mbali mbali ikiwemo na kuchelewa kufika kwa

Washauri Waelekezi kutoka Sudan, ambapo Mkandarasi wa Daya alikuwa ameshaanza kazi na hivyo Mshauri Muelekezi kutokubaliana na kazi iliyofanywa na Mkandarasi wa kati yeye hayupo.

Mhe. Naibu Spika, Mshauri Mwelekezi aliagiza kufanyika uchunguzi wa udongo wa Daya na kupelekwa kwenye Maabara za Chuo Kikuu cha Dar-Es-Salaam kwa uchunguzi, na mgogoro baina ya Mshauri Mwelekezi na Mkandarasi wa Kituo cha Daya ukaanza hapo. Kwa Upande wa Makunduchi, ujenzi ulichelewa kwa sababu zinazofanana na za Daya, lakini kuchelewa ujenzi pia kulichangiwa na Mkandarasi kuwa na kazi nyingi ya ujenzi wa jengo katika Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia na hivyo kuonesha wazi kutokuwa na uwezo wa ufundi na wa kifedha kuendeleza ujenzi wa maeneo mawili kwa wakati mmoja. Kwa sasa ujenzi wa Kituo cha Makunduchi unaendelea na umefikia asilimia 20 na ule wa kituo cha Daya umesimama ukiwa umefikia asilimia 5 tu.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo sasa napenda kumjibu Mhe. Mjumbe kama hivi ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, wizara haikuongeza muda wa Kampuni ya Mshauri Mwelekezi baada ya kumaliza muda mwezi Januari 2018 na badala yake ujenzi wa kazi hiyo utasimamiwa na Wakala wa Majengo ya Serikali kwa muda hadi hapo atakapopatikana Mshauri Muelekezi mwengine. Mkataba wa usimamizi ujenzi baina ya Wizara na Wakala wa Majengo ya Serikali unatarajiwa kusainiwa kabla ya kumalizika mwezi huu na kufuatia na kuanza tena kwa Ujenzi. Kazi za Ujenzi zinatarajiwa kuchukua miezi 18 hadi kukamilika. Kwa vile mkataba wa Mkopo kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika utamalizika mwisho Mwezi Disemba 2018, wizara inakusudia kuomba kuongezwa muda wa kukamilisha ujenzi huo wa Daya na Makunduchi kwa Benki ya Maendeleo ya Afrika. Hivyo, ni matumaini yetu kuwa ombi letu litakubaliwa na hivyo ujenzi utakamilika ifikapo mwezi Disemba 2019.

(b) Mhe. Naibu Spika, kwa sasa wizara inaendelea na mchakato wa kumpata Mshauri Mwelekezi mwengine, katika kipindi hiki cha mchakato huo Wizara itawatumia wataalamu wetu wa ndani kutoka "*Zanzibar Housing Agency* (*ZBA*)" kusimamia ujenzi mpaka atakapopatikana Mshauri Mwelekezi mpya. Pia, wizara imemtaka Mkandarasi wa ujenzi wa kituo cha Makunduchi kuingia mikataba midogo midogo (*sub-contracts*) na kampuni nyingine ili kuwezesha ujenzi kufanyika kwa kasi kubwa zaidi.

(c) Mhe. Naibu Spika, wizara imeunda kamati maalum ya kusimamia utekelezaji wa mradi (*Project Coordinating Unit – PCU*). Kamati hii hufanya ziara za mara kwa mara kwenye maeneo ya ujenzi na pia hukutana kujadili maendeleo ya mradi. Aidha, kamati hushiriki katika vikao vinavyofanyika kila mwezi (*site meeting*) pamoja na wakandarasi na wasimamizi wa ujenzi.

Vile vile, kamati huandaa ripoti ya utekelezaji kwa kila robo mwaka na kuiwasilisha kwa uongozi wa wizara ambao hujumuisha wajumbe kutoka sekta nyingine kama vile Wizara ya Fedha na Mipangon na wizara inayoshughulikia na Ajira kupitia kikao cha kamati ya

uongozi (*Steering Committee Meeting*). Wajumbe wa *SCM* hujadili ripoti, mipango ya mradi na kutoa ushauri kadiri inavyohitajika kwa maendeleo ya utekelezaji wa Mradi. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Ali Khamis Bakar: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ya kuweza kuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba nimuulize swali la nyongeza.

a) Mhe. Naibu Spika, kutokana na kuchelewa kwa ujenzi serikali imeingia hasara kiasi gani?

b) Mhe. Naibu Spika, ni muda gani miradi hii ilitarajiwa kukamilika na hasara hii atalipa nani?

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Naibu Spika, hasara iliyopata serikali kwa sasa ni ya kuchelewa mradi, yaani hasara ya muda na lini limekusudiwa kufanya kuchelewa kufanyika. Kwa hivyo, hapana hasara ya fedha moja kwa moja, isipokuwa ni ya muda wa utekelezaji wa mradi. Ahsante sana.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu marefu, mazuri na ya kisanii katika wizara hii, swali langu nauliza.

Je, ilipelekea vipi mjenzi huyu kuanza taratibu za ujenzi bila ya Mshauri Mwelekezi, kwa sababu bila ya Mshauri Mwelekezi mjenzi hutoweza kufanyakazi. Je, taratibu hizi kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ziko vipi?

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Naibu Spika, kiutaratibu ni kwamba mjenzi hawezi kuanza ujenzi kabla hajafika Mshauri Mwelekezi, huo ndio utaratibu ulipo. Lakini kwa bahati mbaya sana mjenzi huyu alianza kazi za awali ambazo alitarajia kwamba atakapokuja Mshauri Mwelekezi atazikubali.

Mhe. Naibu Spika, hakuanza kazi kienyeji huyu, alianza kazi kwa ku-*test* udongo ambao aliupeleka katika Chuo cha Karume hapa, ukathibitishwa na mambo mengine. Lakini alipokuja Mshauri Mwelekezi yeye akasema haamini, haiamini taasisi yetu kwa hivyo akapeleka kwenye taasisi nyengine, pamoja na kufahamishwa kwamba taasisi hii inakubalika na sisi tunaikubali, lakini yeye alielekeza kufanya vyengine.

Kwa hivyo, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali haina utaratibu mwengine zaidi, isipokuwa ule ule wa kufanyakazi pamoja kwa maelekezo ya Mkandarasi. Ahsante.

Nam. 79

Ulipaji Kodi Kwa Makampuni Yaliyopatiwa Maeneo ya Ardhi

(Mhe. Mjumbe aliyeuliza swali hili ameliondoa)

Nam. 26

Harakati Kwa Ununuzi wa Meli ya Mafuta na Abiria Zanzibar

Mhe. Mussa Foum Mussa – Aliuliza:-

Naipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa uamuzi wake wa kununua Meli ya mafuta na meli ya abiria na mizigo ambapo jumla ya TZSHS. 20,000,000,000 zimetengwa kufanikisha kazi hiyo.

(a) Je, Waziri kazi hiyo imefikia wapi.

(b) Je, meli hizo kwa mara hii zitaundwa wapi na nchi gani.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 26 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeamua kununua meli ya mafuta na meli ya abiria na mizigo kwa jumla ya TZ SHS.20,000,000,000 zilizotengwa kufanikisha shughuli hiyo. Serikali imeamua kuanza kutengeneza meli ya mafuta na mpaka kufikia Machi, 2018 Serikali imeshalipa asilimia 30 ya gharama ya utengenezaji wa meli hiyo.

(b) Mhe. Naibu Spika, meli hiyo ya mafuta inatengenezwa na kampuni kutoka Uholanzi, lakini kiwanda chake kipo China. Kwa hivyo, meli hiyo inatengenezewa China. Maamuzi ya meli ya abiria na mizigo ya wapi itatengenezwa, yatafanyika wakati wa kutengenezwa ukifika. Lakini maandalizi yanafanyika na baada ya kupata na kuridhika wapi itengenezwe serikali itatoa taarifa.

Mhe. Mussa Foum Mussa: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba niulize swali moja la nyongeza.

(a) Mhe. Naibu Spika, ilipoundwa meli yetu ya Mv. Mapinduzi II haikuchukua muda mkubwa kumejitokeza matatizo. Nimuulize Mhe. Waziri je, wamejipanga vipi na uundwaji wa meli ya mafuta ili kuepuka hayo matatizo yaliyojitokeza katika meli ya MV. Mapinduzi II.

(b) Mhe. Naibu Spika, je ni muda gani tunaotarajia meli hiyo ya mafuta itaingia hapa nchini?

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Naibu Spika, kulikotengenezwa meli ya MV. Mapinduzi II siko inakotengenezwa meli ya mafuta. Kwa hivyo, kama kule kulikuwa kuna kasoro huku bado hatujaziona maana meli bado hatujaipokea.

Kwa hivyo, ni matumaini yangu kwamba kama tulifanya kosa huko nyuma basi safari hii tutakuwa tumejifunza na tumepeleka kwahala kuliko sahihi. Kwa hvyo, tumuomba Mwenyezi Mungu iwe hivyo na tusubiri matokeo.

Mhe. Naibu Spika, tumejipanga vipi, hakuna anayetaka kuharibikiwa. Mtu unapokosea unajifunza na unapojifunza unajikosoa, lakini haimaanishi kwamba hutokosea tena. Kwa hivyo, ni imani yangu kwamba safari hii tumejipanga vizuri, na tuombeeni kwa Mwenyezi Mungu, msituombee mabaya maana meli ni zetu sote. Kwa hivyo, ni matumaini yangu kwamba makosa yale hayatatokea tena. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Masoud Abrahman Masoud: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii, nimshukuru Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri. Mhe. Naibu Spika, mimi nina maswali yangu mawili tu ya nyongeza.

(a) Je, suala la ujenzi wa meli hii ya mafuta wamewashirikisha vipi wataalamu wetu wa ndani?

(b) Mhe. Naibu Spika, inasemekana meli ya Mv Mapinduzi II kwa muda mrefu sasa haifanyikazi na inasemekana kwamba tumetumia zaidi ya dolla milioni moja kuitengeneza. Kwanza suala hili ni kweli na ni lini meli hii itaweza kufanyakazi baada ya kurudi matengenezo?

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Naibu Spika, katika ujengaji wa meli kwa kawaida watu huwa wanashirikishwa tangu siku ya kwanza mpaka siku ya mwisho wanakwenda. Kwa meli hii watu wamekwenda tangu kupatana kwenye mkuku na wataalamu kutoka nchini kwetu wanakwenda kwa kushirikiana nao vile vile.

Mhe. Naibu Spika, kutokana na makosa yaliyotokea nyuma hatutaki tufanye tena kama tulipotokea. Kwa hivyo, tunahakikisha kwamba hatua zote zile zinazotakiwa kufuatwa zinafuatwa, yakija yakitokea yatokee sasa kwa sababu nyengine, lakini ufuatiliaji unafanywa hatua kwa hatua kwa kadiri meli inavyojengwa. Kwa sababu wakifika hatua moja wanaripoti wanakwenda watu kuangalia, wakifika hatua ya pili wanaripoti wanakwenda watu kuangalia. Lakini hata hao wanaokuja kuitumia pia wanashirikishwa ili waweze kuja kuimudu vizuri watakaporudi.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu suala la MV. Mapinduzi II, hivi sasa iko katika matengenezo, vipuri vililetwa, waelekezi wamekuja na wanalifuatilia. Juzi tu nilikuwa na mgeni ambaye amefika kuja

kufuatilia utengenezaji wake. Hatua iliyokwishafikiwa ni nzuri na sidhani kama itafika miezi miwili kuanzia sasa hivi haitofanyakazi. Tuko mbali kilichokuwa kimeharibika vyote vimeshabadilishwa, kwa hivyo tutegemee itafanyakazi hivi karibuni.

Nam. 116

Madaktari Wazalendo Kutokukaa Katika Nafasi zao za Kazi

Mhe. Suleiman Sarahan Said – Aliuliza**:-**

Serikali katika kuendeleza juhudi za kuwapatia wananchi wake matibabu na Afya bora, imejenga hospitali za kisasa ikiwemo Hospitali ya Abdalla Mzee Mkoani. Hata hivyo, kuna baadhi ya madaktari, wengine huenda masomoni na wengine huwa hawakai katika sehemu zao za kazi kwa kisingizio cha kukaa mbali na familia zao.

(a) Je, Serikali inalijua hilo na kama inalijua huchukua hatua gani.

(b) Kuna malalamiko katika hospitali ya Mkoani kuwa baadhi ya madaktari wazalendo huwa hawakai katika nafasi zao au wamekwenda masomoni na kuacha nafasi zao. Je, kuna ukweli kuhusu hili.

(c) Je, ni wafanyakazi wangapi walioajiriwa katika hospitali ya Mkoani na wangapi wanaotokea maeneo hayo ya Mkoani.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu**:**

Mhe. Spika, Ahsante kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Afya naomba kumjibu Mhe. Suleiman Sarahan Said suala lake Nam. 116 lenye vifungu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, kwanza naipongeza sana juhudi Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kujenga hospitali za kisasa katika kuhakikisha wananchi wanapata matibabu na huduma zilizo bora.

(a) Mhe. Spika, ni jambo la kawaida kwa madaktari kwenda masomoni na ni kwa lengo la kujiendeleza ili kuweza kuwa makini na kufanyakazi kwa ufanisi zaidi. Wamalizapo hutakiwa kurudi na kuripoti ili kupangiwa kazi hususan hospitali au vituo vya Afya walivyotoka inategemea na mahitaji yaliyopo. Kwa sasa utaratibu unaotumika daktari anapokwenda masomoni sehemu alipoondoka hupangwa daktari mwengine ili shughuli za utoaji wa huduma zisisite

(b) Mhe. Spika, kuhusu daktari kutokuwepo sehemu zake za kazi bila sababu za msingi ni kosa na ni kinyume cha Sheria na Kanuni za Utumishi wa umma. Hivyo hatua za kinidhamu huchukuliwa kwa mfanyakazi yoyote anayethibika kufanyakosa hilo. Aidha

kwa daktari anaekwenda masomoni Idara inayohusika hupanga daktari mwengine ili huduma za Afya kwa wananchi ziendelee kutolewa.

(c) Mhe. Spika, jumla ya wafanyakazi 184, wameajiriwa katika Hospitali ya Abdalla Mzee Mkoani.

Mhe. Spika nasikitika kulieleza Baraza lako tukufu kwamba Wizara yangu haina kumbukumbu ya idadi wala majina ya walikotoka au asili yao kwao waajiriwa hao kwani kimsingi uajiri haufanyiki kwa kuangalia maeneo anayotoka muajiriwa bali huzingatia zaidi sifa zinazohitajika kwa mujibu wa nafasi za kazi na mahitaji ya nafasi zenyewe. Ahsante Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Naibu Spika, nashukuru na mimi nimsifu sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri lakini na swali (a) na (b) kwa nyongeza.

(a) Mhe. Naibu Spika, wagonjwa hukimbizwa hospitali kwa haraka na gari la mgonjwa linapita njia yoyote ile ilimradi mgonjwa yule afikishwe hospitali, lakini anapofikishwa hospitali unaambiwa kwamba daktari hayupo au watu wa *theater* hawapo hasa nyakati za usiku, na Mwenyezi Mungu ametujaalia kama Hospitali ya Mkoani ina timu ya *Chinese* kidogo ina afadhali. Lakini kama Hospitali ya Chake Chake ni kubwa lakini haina timu kama hiyo. Je, ni sababu zipi zinazofanya kwamba usiku kushikuwepo watu wa *theater* na daktari wa zamu ambaye *qualified* kwa matatizo yoyote ambayo yanayotokea hasa ya operesheni.

(b) Mhe. Naibu Spika, ni kwamba tunakuwa na takwimu nyingi za kupunguza ili vifo vya mama na mtoto visitokee au vipungue zaidi, lakini ukikuta mara nyengine hasa Hospitali yangu ya Chake Chake, utakuta mzazi anakimbizwa au yupo pale lakini akifika mzazi katika hali ile ambayo ni kumuokoa mama au mtoto unaambiwa daktari hayupo, lakini cha ziada unaambiwa ama gari haina mafuta au gari ni mbovu ya kumfuata daktari. Ni sababu zipi zinazofikia kwamba gari haina mafuta au gari iwe ni mbovu wakati pale ni hospitali chochote kinaweza kutoweka.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Afya napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swalia lake la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, tatizo hilo tulikuwa nalo sana Wizara ya Afya kipindi kilichopita lakini tunamshukuru Mwenye Mungu na tunaishukuru Serikali yetu ya Mapinduai ya Zanzibar chini ya uongozi wa Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kuongeza Bajeti kuanzia mwaka 2016/2017 na 2017/2018 na kupatiwa kiwango cha kuridhisha na cha kutosha.

Mhe. Naibu Spika baadhi ya matatizo yamepungu sana likimwemo tatizo alilolieleza Mhe. Suleiman Sarahan Said.

Mhe. Naibu Spika, tulikuwa na uhaba sana mkubwa sana wa wafanyakazi katika kipindi cha nyuma na ndio ilikuwa inapelekea akienda mgonjwa huambiwa daktari hayupo wafuatilie, madaktari ni binaadamu, kama binadamu wengine wakawaida na huwa wanahitaji pia wapate mapumziko baada ya kufanya kazi ngumu ya kutibu wagonjwa wengi. Sasa kipindi kile ilikuwa daktari anatoka kwenda kupumzika ili arudi baadae kuja kushughulika, na lakini katika kupumzika kwao huwa wako *standby any time* litokealo lolote wanapigiwa simu na wanakuja haraka ili kuokoa maisha ya wagonjwa.

Mhe. Naibu Spika, tatizo hilo sasa limepungua au siwezi kusema halipo kabisa kwasababu kila mtu ana ubinadamu wake *misunderstanding* zinatokea baadhi ya wakati. Lakini limepungua kwa asilimia kubwa.

Mhe. Naigu Spika, hivyo naomba nikuthibitishie kwa kadri tunavyoendele kusonga mbele na kadiri Mhe. anavyo jitahidi kuboresha Bajeti ya Wizara Afya, basi baadhi ya matatizo mtayaona taratibu yanaondoka na kupatikana ufanisi mzuri zaidi katika kutoa huduma za Wizara ya Afya. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Afya:Mhe. Naiu Spika, naiomba ni mshukuru sana Mhe. Naibu Waziri wa Afya kwa majibu mazuri sana ya nyongeza aliyoelezea, naomba kuongezea jambo moja tu ambalo Mhe. Suleiman Said Saharan ameuliza suala la gari.

Mhe. Naibu Spika, ni kweli kulikuwa na tatizo la gari na mimi mwenyewe bahati nzuri nilifika nikakuta kulikuwa kuna magari mawili mabovu, lakini bahati nzuri sasa hivi moja lishatengenezwa na la pili linategemewa wakati wowote litakuwa linafanyakazi.

(Hapa palitokea matatizo ya mitambo (microphone) zilikuwa na matatizo)

Mhe. Simai Mohammed Said: (Anaendelea kutokana na tatizo la mtambo baadhi ya maelezo yamekosekana)…….. huo ni kukosefu wa fundi wa umeme ambaye kulikuwa kuna fundi mmoja ambaye anasimamia vifaa vyote ndani ya hospitali pamoja na umeme ambao umetokana unaotokana na *ZECO*.

Lakini pia ilikuwa yeye anafanyakazi kwa masaa 24 ambapo hana muda wa kupumzika. Sasa je, kwa hivi sasa mmefanya utaratibu wowote wa kupata mafundi au pengine ma-*Engineers* wengine watakaoweza kusimamia mashine ambazo zinazostahiki. Lakini pia katika tatizo moja ambalo limepita katika suala (b) ni kwamba kulikuwa kuna daktari mmoja tu wa macho ambaye anasimamia wananchi wengi sana wanaotoka maeneo tofauti, ambaye alikuwa anafika pahala daktari huyu mikono yake inakuwa hawezi kufanyakazi inatetemeka hata macho inafika pahala anasinzia kutokana na muda mwingi kukaa na njaa kwa sababu ya kazi.

Je, hivi sasa kuna daktari wengine mumepata wa macho ambao wanaweza kutoa tiba kwa wananchi wa Hospitali hii ya Abdalla Mzee huko Pemba.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naigu Spika, naomba kumjibu Mhe. Simai Mohammed Said sualallake lake lenye (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, upungufu wa fundi umeme katika Hospitali ile ya Abdalla Mzee bado upo kwa sababu fundi ambaye tunae hatoshelezi mahitaji kwa hospitali nzima kwa kila siku, lakini huwa tunatumia mpaka mafundi wa Wizara inayohusika na umeme ili kuondosha mapungufu na kasoro mbali mbali ambazo zinajitokeza katika hospitali ile. Hata hivyo katika jumla ya wafanyakazi ambao tunategemea kuajiri basi pia tunategemea kuajiri mafundi wa umeme watati na kuwasambaza sehemu mbali mbali, tunagemea pale Hospitali ya Abdalla Mzee tutapeleka fundi umeme.

(b) Mhe. Naigu Spika, kuhusu Daktari wa macho naomba kumjibu kwamba sina uhakika vizuri kwamba katika wafanyakazi tuliowaajiri madaktari wa macho wamo au vipi naomba hili nikujibu kwa maandishi

Nam. 163

Utunzaji Wa Takwimu Za Karafuu Na Mazao Mengine Ya Biashara

Mhe. Asha Abdalla Mussa – Aliuliza:-

Katika suala zima la utunzaji wa takwimu za karafuu na mazao mengine ya kilimo Zanzibar.

Je, ni "program" gani inayotumika katika kutunza takwimu hizo.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Biashara na Viwanda naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 163 kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, kwa sasa Shirika bado linatumia mfumo wa kawaida wa uwekaji wa takwimu kwa kutumia *"EXCEL sheets"*, lakini kutokana na umuhimu wa kuwa na mifumo ya kisasa ya kieletroniki Shirika limo kwenye hatua za mwisho za kumpata mtaalamu, wa kuandaa mfumo bora wa uwekaji wa takwimu kwa kutumia mfumo wa kisasa *"Statistical Management Information System"*.

Mhe. Asha Abdalla Mussa: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana kutokana na umuhimu wa kuwa na mfumo wa kisasa ambao tunaweza kutunza takwimu zetu kwa usahihi zaidi na Mhe. Naibu Waziri amesema kwamba shirika limo katika hatua za mwisho za kupata mtaalamu wa kuandaa mfumo huo. Nataka kujua kwamba ni muda gani ambao utachukua kuhakikisha kwamba mfumo huu utamalizika kwa haraka.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako na kwaniaba ya Waziri wa Biashara wa Biashara na Viwanda naomba kumjibu Mhe. Asha Abdalla Mussa kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, mfumo huuambao tunaoutayarisha utakuweko katika bajeti hii tunayoipisha mwaka huu. *(Makofi)*

Mhe. Nadir Abdul–latif Yussuf: Mhe. Naibu Spika, Bismilillahi-Rahmani Rahiym, nakushukuru naomba kumuuliza swali la ziada lenye (a) na (b) Mhe. Naibu Waziri wa Viwanda na Biasharan na Masoko kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa Karafuu yetu ni nzuri sana na inasifika duniani naomba unieleze kwamba karafuu yetu ina *grade* gani katika karafuu za dunia ni *top one, two* au katika *top-ten,* tuko namba ngapi katika *grade* ya karafuu yetu ya Zanzibar.
(b) Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar mnauza sana karafuu ni nchi ngapi ambazo mna-*supply* karafuu zetu kwenda huko nchi za nje na nchi ngapi ambazo zinatambua karafuu yetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda:Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusu yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Biashara na Viwanda napenda kumjibu Mhe. Nadir swali lake kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, kwanza suala mama linatokana na takwimu za mazao ya karafuu lakini kwa faida yake nitaomba kumjibu kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, mwenyewe Mheshimiwa kakiri kwamba karafuu yetu ni *top*, lakini pia anauliza kwamba je, karafuu yetu. Kwa hivyo Mheshimiwa karafuu yetu ndio karafuu ndio miongoni mwa karafuu ya mwanzo dunia, ndio maana ina soko, ndio maana na serikali tunalihamasisha kikamilifu kuhakikisha karafuu yetu tunailima kwa wingi ili nchi yetu na wananchi wetu wapate kuneemeka.

(b) Mhe. Naigu Spika, kutokana na umuhimu na ubora wa karafuu yetu nchi nyingi zimekuwa zinazitaka karafuu zetu kwa sabau ni karafuu bora na ni karafuu nzuri.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda kwa ruhusa yako naomba kuuliza suala la nyongeza:-

Mhe. Naibu Spika, utunzaji wa takwimu ni jambo muhimu sana kwa karafuu kwa karafuu zetu na mambo mengineyo au mazao mengineyo. Lakini kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri alipojibu alisema tu kwamba shirika au Wizara ipo mbioni kutafuta mtaalamu wa mfumo wa kisasa. Je, mtaalamu huyo tunategemea anatoka nchi gani na ubora wake uko vipi.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusu yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Biashara na Viwanda napenda kumjibu Mhe. Ali Suleiman Ali swali lake kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, mtaalamu huyo atatoka katika nchi gani.

Mhe. Naibu Spika, katika taratibu za kumpata mtaalamu muelekezi za serikali hazitegemei nchi lakini tuna–*prefer* Mzanzibari au Mtanzania. Kwa hivyo tutapotangaza yule atakayekuwa ana sifa za kuweza kufanyakazi hiyo ndio atakuwa mu-*award* ile kitu Mheshimiwa.

MUONGOZO WA SPIKA

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kunipa nafasi hii ukanisaidia kupata muongozo.

Mhe. Naibu Spika, leo katika *order paper* tuliwekewa Hati zilizowasilishwa Mezani. Kuna Hati ya Waziri wa Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kuhusu Ripoti ya Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali. Lakini pia katika Hati zilizowasilishwa kuna Hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza Hesabu za Serikali (*PAC*). Sasa muongozo wako ninaoutaka.

Ninataka nijue kwamba umeshaipata Ripoti ya Hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC* na kwa sababu kuwasilisha kitu ambacho hakipo ni kinyume cha taratibu zetu za Baraza la Wawakilishi. Kwa sababu pia hii Ripoti ya Mwenyekiti na sisi tulikuwa tunataka tuione ili tuone zile *comments* ambazo walizozitoa. Sasa hofu yangu tusije tukawasilishiwa Hati hewa ambayo haijaandikwa na sisi tukapitisha katika *order paper* ya leo. Kama hilo halijafanyika basi mimi nitaomba Mhe. Naibu Spika, basi katika *order paper* ya leo isifuatwe kama ilivyo, kwa sababu nina wasi wasi Kamati ya *PAC* haijakaa wala hiyo Ripoti ya Mwenyekiti au hotuba yake ambayo wamesema imewasilishwa Barazani haijakuwepo.

Mhe. Mwenyekiti, ahsante,

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Hamza sijui wasi wasi wako ni upi wakati mwenyewe Mhe. Mwenyekiti wa Kamati wa Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali tayari ameshaweka Mezani. Sasa labda tumuachie Mhe. Waziri alijibu, Mhe. Waziri wa Katiba na Sherir na Utumishi wa Umma, alijibu hilo lakini tayari imeshawekwa mezani.

Tunaendelea na shughuli yetu.

Waheshimiwa Wajumbe kwanza kabisa nina matangazo mawili mbele yangu na nilikuwa naomba nitoe matangazo hayo na matangazo yenyewe ni shukurani kutoka Jumuiya ya Wachangiaji Damu na tangazo la pili ni la ugeni ambao leo umekuja hapa ndani ya Baraza la Wawakilishi.

Sasa naomba nisome shukurani hizo kutoka kwa Jumuiya ya Wachangiaji Damu. Waheshimiwa Wajumbe nachukua fursa hii kukushukuruni na kukupongezeni sana kwa kujitokeza kwa wingi katika bonanza letu la uchangiaji wa damu, tulilolifanya juzi Jumamosi tarehe 12/05/2018 na Waheshimiwa Wajumbe mkachangia damu hiyo.

Aidha kwa kipekee na umuhimu mkubwa napenda pia kuwashukuru watendaji wetu wa Baraza wakiongozwa na Katibu Bi. Raya Issa Msellem na hususan Kamati ya maandalizi pamoja na wananchi wote waliojitokeza kutuunga mkono kuja kujumuika nasi katika zoezi hili.

Waheshimiwa Wajumbe kwa furaha napenda kuwajulisha kwamba zoezi letu limefanikiwa kwa 200 kwani makisio yetu yalikuwa ni kuchangia chupa 55 na badala yake tumevuka lile lengo na kufanikiwa kuchangia chupa 101. Kutokana na hatua hiyo nzuri kabisa Jumuiya ya Wanachama wa kuchangia Damu Zanzibar imetutunukia cheti cha shukurani kwa kukuunga mkono shughuli za uchangiaji wa damu.(*Makofi*)

Waheshimiwa Wajumbe naomba sasa niwaoneshe cheti chetu cha shukurani hizo ambacho ni hili hapa na nitaomba wasaidizi waje wakitembeze kwa Wajumbe wengine, vile vile nawaomba sana tuwe na utamaduni wa kuchangia damu kila inapowezekana na pia kuwahamasisha wananchi katika majimbo yetu ili kuhakikisha kwamba muda wote kunakuwa na damu ya kutosha katika benki yetu. Ahsanteni sana kwa kunisikiliza.

Tangazo la pili, hili ni la wageni wetu waliofika hapa Barazani leo ambao hao ni wageni hao ni wa Mhe. Mahmoud Thabit Kombo, Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale. Ni ujumbe maalum kutoka Ufalme wa Nchi ya Oman ambao umekuja kwa lengo la kufanyia matengenezo makubwa jengo la Beit el Ajaib na jengo la *People's Palace*.Wageni hao ni Mhe. Salum M. Al Mahrouk ambaye ni Katibu Mkuu Wizara ya Utamaduni na Mambo ya Kale nchini Oman na Bwana Hussein Al Abry pamoja na Dkt. Ahmed Hamoud Al Haps Balozi Mdogo wa Oman hapa nchini.(*Makofi*)

Waheshimiwa Wajumbe kwa mujibu wa taarifa ambazo amenipa Mhe.Waziri Anayehusika, amesema kwamba wamekuja kwa lengo la kutia saini mkataba wa ukarabati wa majengo hayo ambapo baada tu ya kusaini hayo makubaliano, kazi hiyo katika jengo hilo mashuhuri Barani Afrika na muhimu katika urithi wa kimataifa ulimwenguni, kazi itaanza mara moja (*Makofi*).

Niwashukuru sana tuwashukuru sana Serikali ya Oman kwa kuja kutuunga mkono katika masuala yetu mbali mbali na niwakaribishe sana tena ndani ya Baraza la Wawakilishi pamoja na wasaidizi wote ambao wamekuja nao.

Nawashukuru sana kwa kunisikiliza Waheshimiwa Wajumbe. (*Makofi*)

Mhe. Wajumbe kuna wachangiaji saba.

Samahani kuna wageni wengine nimekuwa- *carry out* ya hawa wageni ambao wamefika. Kuna wageni wengine kwa ajili ya ziara ya kimafunzo. Kuna vijana wetu wamekaa pale wapo na ni wanafunzi kutoka *Salahi Islamic* ya Mwanakwerekwe Mkoa wa Mjini/Magharib. Jumla yao ni arobaini na walimu watano wakiongozwa na Bi. Aziza Abdalla pamoja na Rais wa wanafunzi wa skuli hiyo ndugu Idrissa Mussa Haji.

Karibuni sana vijana wetu.(*Makofi*).

Sasa Waheshimiwa Wajumbe kama nilivyosema tuna wachangiaji wengine saba, ilikuwa matarajio kwamba tunaweza tukapitisha vifungu mchana huu lakini kutokana na kwamba wamekuja wachangiaji wengine zaidi. Kwa hivyo inawezekana sana kwamba vifungu tutapitisha jioni.

Sasa kabla ya kuanza utaratibu nitamwita Mwenyekiti Mhe. Mwanaasha Khamis Juma aje aendelee na shughuli yake hii iliyobakia.

Mheshimiwa karibu.

(Hapa Mhe. Mwenyekiti (Mwanaasha Khamis Juma) alikalia kiti)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe majadiliano yanaendelea sasa naomba nimwite Mhe. Mohammed Said Mohammed Dimwa atafuatiwa na Mhe. Miraji Khamis Mussa na Mhe. Bahati Khamis Kombo ajiandae.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru sana na nikishukuru kiti chako kwa kuwa leo mimi ndiyo mchangiaji wa mwanzo, lakini kubwa zaidi nimpe pongezi kubwa sana ndugu yangu Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Baraza la Mapinduzi Mhe. Issa Haji Ussi Gavu, kwa uwasilishaji wake mzuri sana lakini nimwambie tuendelee kuwa pole kwa kipigo tulichokipata pia jana tutafika tu.

Mhe. Mwenyekiti, Pia niwape pongezi kubwa sana na niwashuru ndugu zetu wa kamati hii ya kusimamia viongozi wakuu wa serikali kwa kuendelea kukubali kila kitu wanachokiona kinafaa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianze mchango wangu kwenye ukurasa wa 9 kwenye namba 24 miradi mingine aliyoitembela Mhe. Rais, nimpongeze sana Mhe. Rais kwa kutembelea miradi mingi sana lakini kubwa tunaloliona manufaa ambayo tunayapata kwa kutembelea. Moja katika hiyo miradi ambayo alitembelea alisema alitembelea Ras el Khaimah na kulikuwa na maendeleo ya kuweka maelewano *MOU* yaliyotiwa saini tarehe 12/11/2011, vile vile jitihada za pamoja za baina ya Ras el Khaimah na Zanzibar zitaendelezwa lakini na kufanya utafiti wa mafuta.

Mhe. Mwenyekiti, juzi nilipokuwa nikichangia, hotuba ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, kwenye gesi na mafuta Mhe. Waziri baadae wakati ana-*wind up* alisema kulikuwa na makubaliano, lakini vile vile hakunambia ni makubaliano gani, lakini humu kwenye kitabu cha Mhe.Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi anasema ulikuwa na *MOU* na yeye Mhe. Issa Haji Ussi ni Mwanasheria nguli. Sasa nataka kujua *MOU* ni makubaliano ambayo tunasema ni *Gentleman agreement* wakati wowote yanaweza yakavunjika na kwa sababu gani kitu hiki ni kikubwa kwa nini tutie *agreement* tusitie *contrac*t ikawa *forced by law*.

Sasa nilikuwa nataka ufafanuzi tu atakapo kuja hapa anieleze kwa sababu zipi kitu cha utafiti ni kitu kikubwa siyo cha kutia *MOU, MOU* ni makubaliano tu ya kawaida hata tukizungumza mimi na wewe Mwenyekiti tukishakubaliana tunaweza tukaandika tu *MOU* ya kitu chochote kile.

Lakini sasa nataka kujua je, jambo hili lilikuwa halipaswi kuweka *contract* ya kudumu ya jambo la utafiti, jambo la nchi, jambo hili ambalo la wananchi wote.

Mhe. Mwenyekiti, niendelee kwenye namba 26 ukurasa wa 10 katika mwaka wa fedha huo uliotumika hapa, Rais alitembelea pamoja na Kiwanda cha Mahonda ambacho kimeboreshwa na kutiwa mashine mpya tunampongeza sana Mhe. Rais kwa kazi zake kubwa sana ambazo anazifanya, na anatembelea miradi yote ambayo tumesema sasa tunairudisha.

Juzi nilitaka niseme tu na nikasema kuwa hii Sera ya Viwanda ni yetu Zanzibar. Nilikuwa napata ukakasi tu kwa sababu bajeti tuliyoweka lakini hata hivyo jinsi ya soko la viwanda Zanzibar *population* yake ni ndogo sana. Nikakitaja Kiwanda cha Mahonda ambapo kina tani kadhaa zimebaki kule bila ya kuwa na soko, lakini wenzetu ndugu zetu wa damu jana katika magazeti ya leo wametangaza tani 70,354 za sukari wamepewa vibali nje ya nchi.

Sasa ukakasi wangu kuwa soko letu la Tanzania kuweka angalau kuwapa tani 1000 Zanzibar kuingiza pale inakuwa shida. Na nikaeleza wasi wasi wangu sana kwenye uchumi wetu sasa hivi lazima tuingie katika uchumi wa visiwa, kwa sababu wenzetu kila pahala. Mdogo wangu Hamza alisema hata mivao kumi ya khanga basi inazuiwa. Sasa hili la kulitizama zaidi ili tuone basi umakini hapa umejengeka ipasavyo sana.

Lakini jengine niingie kwenye ukurasa wa 18, 47 ambayo inazungumzia hapa Kitengo cha Mawasiliano Ikulu. Mhe. Mwenyekiti, Rais amefanya ziara nchi za Uarabuni kwa kipindi kirefu na tumeelezwa mafanikio yake makubwa sana na sisi tunampa pongeza sana, lakini tangu mimi kuingia Barazani, hii ndio mara ya kwanza kabisa kuweza kupata *update* za mara kwa mara za Mhe. Rais anavyokwenda, shughuli zake anavyozitekeleza kiukamilifu. Nawapa hongera sana.

Lakini hili limezaa ndugu yangu Simai Mohammed Said wakati na mimi tuko katika Kamati ya Viongozi Wakuu tuliwashauri na ushauri huu nadhani umechukuliwa vizuri. Sasa ndiyo matunda yake. Sasa nimpongeze sana Mkurugenzi kwa kazi kubwa anayoifanya ya kumtangaza Mhe. Rais kila kitu na maagizo yake ambayo anayatoa tunaweza kuyapata. Lakini pili nipende kupongeza kwa dhati sana idara hii na watendaji wote siyo Mkurugenzi tu.

Mhe. Mwenyekiti, taarifa mbali mbali tumekuwa tukizipata sana na tunafurahi sana kutokana na kazi kubwa ambayo tunaweza kupitia, lakini nataka kuwa na wasi wasi mwengine jinsi Mhe. Rais anavyotekeleza zile ahadi zake na anapokwenda kutoa majukumu. Lakini utekelezaji wa haya maagizo yote yako vipi. Je, sekta nyengine zinafuata ili tuweze kujua kama ziara za Mhe. Rais zina uzito wake wa kusikiliza utekelezaji, lazima utekelezaji usikilizwe na tuweze kuuona baada ya Mhe. Rais kutoa maagizo, hawa viongozi wengine wanatoa utekelezaji wake, ndio nilitaka nijue.

Mhe. Mwenyekiti, naomba Waziri atueleze je, kuna Kamati yoyote ambayo ina ratibu ziara hii ya Mhe. Rais. Lakini jengine kuna utaratibu wowote wa kutoa taarifa kwa wananchi kuhusiana na utekelezaji wa makubaliano yaliyofikiwa kwenye ziara hizi. Mhe. Mwenyekiti, kwa nini viongozi wengine wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hawafuati utaratibu wa Dkt. Ali

Mohamed Shein wa kutoa taarifa kwa waandishi wa habari mara baada ya kupewa maagizo yale na kuyatekeleza ya kikazi. Nilikuwa nataka nione Mhe. Waziri akija aniambie jambo hili.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye *program* ya Kuratibu Ushirikiano wa Kikanda na Ushirika wa Kimataifa wa Wazanzibari wanaoishi nje ya nchi. Mhe. Mwenyekiti, hapa nimeona matumizi madogo sana ambayo wamewekewa na kutokana na uzito wa mambo yenyewe, lakini nitakuja kwenye kitabu cha bajeti sasa hivi nitaingia huko ili nione jinsi gani tunaweza tukafanikiwa, lakini niende kwenye ukurasa wa 47 *program* ya Utumishi.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa na Sheriaa ya Viongozi Wakuu wa Serikali baada ya kustaafu. Sasa nilikuwa nimemuomba Mhe. Waziri au Mwanasheria Mkuu atusaidie, kwa sababu sheria hii tuliipitisha Baraza la Wawakilishi na kutiwa saini na Dkt. Ali Mohamed Shein tarehe 28/05/2012. Sasa nilikuwa napata ukakasi juu ya mambo mawili ambayo nitayataja hapa.

Moja katika 34 "*benefit conferred by the Entire Political Leader* ambayo *marginal note* yake inasema *benefit of the Political Leader.*

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa na wasi wasi sana kwa sababu hizi *benefits* zote hapa zimetajwa vizuri lakini wasi wasi wangu kuwa hazifuatwi kikamilifu au tunataka tupate marekebisho, kwa sababu Spika wetu ambaye ndiye chombo hiki anakiongoza anapo-r*etire* hapati *benefits* kama nitakapozieleza huko mbele.

Mhe. Mwenyekiti, nije kabisa ambayo nataka kutoka *second and third schedule*. Mwanasheria Mkuu naomba unisikilize vizuri ukija unipe kwa sababu nina nia. Mhe. Mwenyekiti, nina nia ya kuzuia fungu la Utumishi na Uendeshaji ikiwa sikupata majibu mazuri hapa. Nina nia kubwa sana hiyo, kwa sababu kwenye ukurasa wa 8 wa sheria ile namba ndogo ya 3 inasema, "*amendment of the appropriate minister may from time to time".* Mhe. Mwenyekiti, naomba nirudie tena, *minister may from time to time in consultation with the President or Chief Secretary amends the schedules of this Act by order published in the Gazette*.

Sasa ningemuomba Mhe. Waziri hili akae na Mhe. Rais, ili waone na Katibu Mkuu Kiongozi, a*mendment* ambayo wataifanya ili basi na Mhe. Spika wetu *retire* aweze kupata mafanikio hayo na kama inavyosema hapa *Second Vice President* anapo-*retire* yametajwa mambo yake mengi, ambayo nitayasoma kidogo ambayo Mhe. Spika anayakosa.

Moja "*one person assistant.* Spika wetu anapokuwa anastaafu hapati mtu wa kumsaidia na tumemshuhudia anakwenda nje, anakwenda mpaka kwenye mikutano hata ya Kitaifa ya ndani lakini Baraza linaji-*force* kwenda kumpa mtu na hii inaweza kuwa *audit query* na sisi tunaweza tukamuuliza Katibu wa Baraza, hebu tuambie pesa hizo unazipata wapi. Lakini Sheria hii ikiwekwa sawa basi itakuwa vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, lakini jengine anasema Makamu wa Rais anasema, *Personal Doctor* hapati Mheshimiwa Spika wetu. Lakini jengine *House accommodation and medical care to pay by the government.* Hii hakuna sasa tungemuomba Mhe. Waziri ajaribu sana kulipitia suala hili na atwambie.

Lakini *third scold* ambayo inasema *benefit of former speaker*. Sasa nimeanza kuzitaja pale. Mheshimiwa utakapokuja uniambie Sheria hii tumekwenda vipi ili basi tuone na sisi Mhe. Spika wetu amefanya kazi kubwa ya kutumikia Baraza hili.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye kitabu. Sasa nitakwenda kwenye kitabu tofauti na mambo mengine. Mheshimiwa kwenye kitabu naomba Mhe. Waziri achukue kitabu kwa vizuri sana nataka kwenda kwenye fungu A01 katika ukurasa wa 3.

Mheshimiwa. kuna mwisho kabisa kunasema maoni ya wananchi kuhusu taarifa zinazotolewa na Mhe. Rais.

Mheshimiwa unapopanga vitu hivi kunakuwa na shabaha au *target* sasa hapa hapana *target* ya ku- *plain* chochote sio kwa mwaka 2017/2018/2019 mpaka 2020 hakuna *target*, lakini mimi nilikuwa naona haya ni kweli hayana *target* lakini jambo hili linapimwa kwa *qualities* huwezi kupima kwa namba maoni haya ya wananchi. Sasa nione tu Mhe. Waziri aniambie ni kwa sababu ipi hatujaweza kuweka hapa, pengine amepitikiwa au laa.

Mhe. Mwenyekiti, tuendelee kwenye ukurasa wa A04 hapa katika *Column* ya pili pana Idara ya Uhusiano na Ushiriki wa Kimataifa, kuratibu ushiriki wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika mikutano ya kikanda. Mhe. Mwenyekiti, hapa hapakupangwa pesa yoyote sikuona kupangiwa chochote, lakini huku nimeona kupangiwa mikutano 48 ndio nikasema pesa zile ambazo zilitengwa huku ni pesa kidogo sana, lakini nitakuja kuongeza fungu na nitalizuia fungu huku moja ili tuweze kuongeza tuweze kufanya mikutano hii mingi sana.

Lakini jengine katika ukurasa huo huo kuna Idadi ya Mikataba ambayo Zanzibar na Tanzania imesaini kwa mtengamano wa kikanda na kimataifa. Sasa mwaka jana haikutengwa yoyote hapa sioni kutengwa chochote. Lakini mwaka huu imetengwa mikataba kumi sasa nilikuwa najiuliza panahitaji maelezo ya kina hapa kutaka kujua mikataba hii ya mwakani kumi, wakati 2017 hakukuwa na chochote kigezo gani lilichokifanya tuweke *target* ya mikataba kumi, mimi nilikuwa nataka kujua tu kwa urahisi sana.

Lakini kuna idadi ya miradi ya maendeleo ambayo imefanikiwa kupata kutokana na ushiriki wake huo wa kimataifa imetekelezwa vipi, nilikuwa nataka kujua pametekelezwa vipi hapa kwa sababu katika suala hilo Zanzibar mikataba iliyosainiwa Zanzibar imetekeleza kikamilifu. Kwa mfano kuna mkataba wa Maputo ambao ninao nitamuomba msaidizi aje achukue ampelekee Mhe. Waziri, mkataba huu wa maputo ambao nchi hizi za Afrika za *AU* zilikuwa na makubaliano kutenga pato la asilimia kumi kwa sababu ya kilimo. Sasa Zanzibar imetenga vipi nilikuwa nataka kujua na nataka nimpe mkataba huu ambao nimeuchukua kwenye *net*.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, twende tena kwanye ukurasa wa AO5 idadi ya watumishi waliopatiwa mafunzo kwa muda mrefu, nilikuwa nikitizama sana kitabu hichi idadi ya watumishi waliopatiwa mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi haiowani na ile iliyoandikwa katika kitabu cha hotuba ya Mhe. Waziri. Ninaomba Mhe. Waziri arudi kwenye kitabu chake katika ukurasa

wa 61 na 62 katika kiambatanisho 4 haiowani kabisa na kwenye kitabu hichi kikubwa. Kwa hivyo hapa Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa naomba maelezo ya kina kabisa.

Halafu ningeomba vile vile turudi kwenye ukurasa wa sita ukurasa wa AO1, wafanyakazi waliofanyiwa upekuzi, humu inasema wafanyakazi waliofanyiwa upekuzi ni 80 lakini na *target* ya mwakani ni 200, lakini kwenye kiambatanisho hichi kina zaidi ya elfu mbili sasa haviowani. Ningeomba Mhe. Waziri atakapokuja atuweke tu kidogo tujue tunachokifanya kitu gani.

Mhe. Mwenyekiti, naendelea mbele kwenye kifungu hichi hichi AO1 ambacho fungu la matumizi ya Serikali. Kifungu kikubwa PA 0101 kifungu kidogo SA 010101 kusimamia huduma na kushughulikia Mhe. Rais. Mhe. Mwenyekiti, fungu hili nilikuwa nikiomba tu maelezo kidogo naona kidogo safari hii limenona sana sasa nilikuwa nataka kujua kwa nini limenona sana.

Lakini kifungu kidog cha HA 01010101 Kuratibu usimamizi wa Shughuli za Mhe. Rais, fungu hili lilikuwa limenona sana katika kipindi cha mwaka jana lakini mwaka huu limepungua. Je, shughuli za kumsimamia Rais zimepungua au kuna mafanikio gani hata zikapungua nilikuwa naomba ufafanuzi.

Lakini kifungu kidogo cha HA 01010102 Kusimamia Ikulu na nyumba za Serikali. Mheshimiwa tulitizame hilo fungu limezidi zaidi ya mara mbili lilikuwa na milioni 730, safari hii lina bilioni 2,475,000,100,000/=. Sasa mimi nilikuwa naomba maelezo ya kina kuweza kujua hapa.

Lakini fungu jengine kifungu kikubwa cha SA 01 *(Hapa microphone iligoma)* imefanyika lakini nilikuwa naomba maelezo ya kina niweze kuyapata.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu chengine ambacho nitakwenda Mheshimiwa ikifika dakika mbili uniambie maana nataka nizuie baadhi ya mafungu usije ukanambia muda wako umekwisha moja kwa moja.

Mhe. Mwenyekiti nakwenda kwenye kifungu kikubwa cha PA 010102 kifungu kidogo cha SA 010201, kuratibu shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kikanda. Sasa ndio maana nikasema mwaka jana wamepangiwa milioni 306,000,386,000/=. Safari hii wamepangiwa milioni 359 ni kiasi kidogo sana. Sasa nilisema hichi nianze kukipunguza na nianze nitakuelekeza wapi kuna fungu la kuweza kulipangua.

Mhe. Mwenyekiti, nije tena kwenye kifungu kidogo AO 10202 Kuratibu Shughuli za Wazanzibari wanaoishi nje ya nchi. Mheshimiwa hii kuratibu naona ni kazi kubwa sana na pesa hivi zimepungua tofauti na za mwaka jana. Kwa hivyo nilikuwa nataka nimuombe tu Mhe. Waziri anipe ufafanuzi wa kutosha sana. Lakini Mhe. Mwenyekiti, kuna fedha za maendeleo kwenye ukurasa wa AO 114 kuna fedha za maendeleo kusimamia Ikulu na Nyumba za Serikali na kuimarisha nyumba za Serikali na Ikulu ndogo, nilikuwa nataka kutoa neno hapa.

Mhe. Mwenyekiti kwa mujibu sasa wa taratibu na *geographical* yetu mimi naona nataka niishauri hakuna haja ya kuweka Ikulu ndogo ndogo, kwa mnasaba gani. Pemba peke yake kunataka kujengwa Ikulu nne ambazo tatu zimekamilika na moja ya Micheweni. Sioni haja kwa

sababu bado tunao uwezo wa kufika rahisi, kuna Ikulu Wete, lakini kuna Ikulu Mkoani lakini kuna Ikulu na Chake Chake. Sasa sioni haja pesa zote hizi kuanza kuzitumia huko kuliko kwenda kwenye mikutano ya kimataifa.

Kama hapa Zanzibar kuna Bwefum, lakini kuna Mkokotoni, sifikirii kama Mhe. Rais hata mara moja anakwenda kutembea na kupumzika … *(Hapa microphone iligoma)* tu-*save* kuweza kuwatumikia wananchi zaidi kuliko hivyo. Sasa Mhe. Mwenyekiti, fungu hili nitalizuia na fedha hizi nitaziongeza nyengine kwenye fungu lile la uratibu wa Wazanzibari nje ya nchi ili kuona hapo, nina nia ya kuzuia na kutoa shilingi yangu ikiwa sitopata majibu ya kutosha.

Mhe. Mwenyekiti, niunge hotuba hii mkono kwa asilimia thamanini lakini asilimia ishirini nisubiri mpaka Mhe. Waziri atakaponipa majumuisho ya mambo yangu haya na nina nia ya kuiondoa shilingi kwenye Ofisi hii. Mhe. Mwenyekiti nikushukuru sana. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana nakushukuru Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa). Sasa naomba nimuite badala ya Mhe. Miraji naomba nimuite Mhe. Bahati Khamis Kombo na Mhe. Shehe Hamad Mattar ajiandae.

Mhe. Bahati Khamis Kombo: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kuniona kwanza kabisa nimpongeze sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa juhudi zake kubwa anazochukua ili kuwasaidia wananchi kuwaondolea matatizo mbali mbali.

Lakini pia nimpongeze sana Mhe. Waziri vile vile kwa mashirikiano mazuri aliyokuwa nayo katika kusaidia wananchi wetu, vile vile niwapongeze washauri wa Rais kwa juhudi zao wanazozichukua kumshauri vizuri Rais ili kuweza kuitekeleza vizuri Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitasema kwa ujumla na nitasema madogo sana kama dakika tatu tu zinanitosha. Mimi kwanza nimpongeze sana Mhe. Rais kwa kuwajali vijana kuwaletea Baraza la Vijana, uhuru ambao aliwapa vijana ili na wao kuona kwamba Mhe. Rais hakuwaacha nyuma na leo wanaendeleza Baraza lao la Vijana. Hivi karibuni tu tumeshuhudia katika Baraza letu hili hili tukufu wamekuja vijana na wakaweza kuzungumza mambo yao kwa ufasaha mzuri zaidi, kwa hivyo tunampongeza sana Mhe. Waziri.(*Makofi*).

Lakini vile vile Mhe. Mwenyekiti, nije katika suala zima la maji safi na salama, Mhe. Rais kwa kweli anafanya mambo mengi sana na anapata fursa nyingi sana za kwenda kwa wenzetu na akirudi tu anatuletea zawadi nzuri ikiwemo maji safi na salama. Hivi karibuni tumeshuhudia kwamba sisi sote kaleta visima vingi sana ambavyo amevipata kwa wenzetu wa China, wamekuja hapa na visima hivi vipo vingi katika maeneo tofauti tofauti.

Mhe. Mwenyekiti, tuje katika suala la elimu bure elimu bure. Mhe. Rais …

(Hapa microphone iligoma)

Mhe. Bahati Khamis Kombo: Nikiendelea mbele vile vile hapa Mhe. Rais alikuwa akitusikiliza tulikuwa tukipiga kelele sana Wawakilishi hatuna walimu, lakini juhudi za makusudi amezifanya kuonana na viongozi na wanachama wa chama cha walimu kuwauliza nini hasa tatizo hata wanafunzi wakaweza kufeli kwa asilimia kubwa. Lakini jibu alilolipata ni kwamba walimu walikuwa ni kidogo. Lakini na yeye Mhe. Rais alichukua juhudi ya kuona kwamba awasilikilize na tayari katupa walimu mia nane wanaendelea kuajiriwa siku hadi siku. Hii ni faraja kubwa ya Mhe. Rais, naye tunamuomba Mwenyezi Mungu amjaalie imani zaidi pale ambapo tunakwama aweze kutukwamua.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea katika suala la barabara mimi nimpongeze sana Mhe. Rais kwa kweli wamefanya juhidi kubwa sana kama alivyozungumza Mhe. Shaibu hapa juzi kwamba wenzetu wa Ng'omeni walikuwa na matatizo makubwa sana ya maji, barabara, afya na umeme. Lakini hivi sasa ukenda Ngomeni ni mjini kushinda hata huo mji wa Chake Chake kunang'ara.

Mhe. Mwenyekiti, tukiendelea vile vile tukitizama wenzetu wa Mgonjoni Mkoa wa Kaskazini (B), vile vile na wao walikuwa na matatizo lakini siku hadi siku Mhe.Rais anaendelea kuwaondolea matatizo mbali mbali, pamoja na kuweko na changamoto za barabara lakini suala hili kwa kweli analisimamia kuona kwamba wananchi wake wanapata maendeleo siku hadi siku.

Mhe. Mwenyekiti, tukiangaliwa Mtambwe kulikuwa hakuna maji, hakuna umeme, hakuna barabara. Lakini hivi sasa maji safi na salama yapo, umeme upo mpaka Fundo na barabara alhamdulillahi tunamshukuru Mwenyezi Mungu, yule mwenzetu aliyesema kwamba akipata madaraka Zanzibar ataifanya kama Singapore, tukiangalia imemshinda Mtambwe kweli ataiweza Zanzibar nzima, tunamwambia kwamba amuangalie Dkt. Ali Mohamed Shein jinsi gani anawaletea maendeleo wananchi wake ili na yeye aweze kuiga.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea mbale niseme tu kwamba nampongeza sana Mhe. Rais na pia namuomba Mhe. Waziri wetu ambae Mhe. Rais kamuamini, afanye juhudi za makusudi kuona kwamba zile changamoto zilizomo kwa wananchi, lakini pia na ahadi ambazo kuwa kaziweka Mhe. Rais basi azisimamie ili ziweze kutekelezeka.

Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru Mhe. Bahati kwa mchango wako. Sasa naomba nimuite Mhe. Shehe Hamad Mattar akifuatiwa na Mhe. Waziri Asiye Wizara Maalum Mhe. Said Soud na Mhe. Rashid Ali Waziri wa Kilimo ajiandae.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa fursa hii sina budi nimshukuru Mwenyezi Mungu naomba aniwezeshe niweze kuchangia hotuba hii ya Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa ufasaha zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nitoe shukurani zangu za dhati kumpongeza Mhe. Waziri jinsi ya uwasilishaji wa ripoti yake, lakini pia niwapongeze wale waliomsaidia katika kuandaa hotuba hii. Niendelee kuipongeza pia Kamati ya Usimamizi ya Viongozi Wakuu ambao kuwa michango

yao kila kukicha inaleta ufanisi katika kuona kwamba Afisi hii inafanya mambo yake ipasavyo, ikiongozwa na Mheshimiwa mahiri Mhe. Omar Seif Abeid.

Kwanza Mhe. Mwenyekiti, Rais wetu ana kila sifa za kuweza kumpongeza kwa yale ambayo kuwa ameyafanya nchini mwetu, baada ya maelezo mengi ambayo kuwa yametolewa pamoja na kwamba wengine washikilia kuzuia vifungu, lakini ni imani yangu kwamba Mawaziri watatoa maelezo vizuri na kuweza kumpitishia vifungu vyake kama alivyoomba, naomba sana wenzangu tuchangie lakini tusizuie vifungu baada ya kupata maelezo. Waziri ajipange.

Mhe. Mwenyekiti, Rais wetu kwa kweli ni Rais bora sana anayejali watu ni kiongozi muungwana anayetimiza ahadi, anayejali wananchi wa katika sehemu hii ya visiwa hivi bila ya kubagua huku na huku. Kwa hivyo ni kiongozi wa mfano katika Afrika ya Mashariki ambaye kuwa kwa sasa hivi anapigiwa mfano, ingawa kuna wengine wanabeza juhudi hii anayoifanya kusema kwamba Rais wetu yuko laini sana, lakini kuwa hivyo haina maana kwamba yeye anajitahidi uvumilivu huu ni sehemu ya utawala bora. Rais wetu anajitahidi kuwa ni sehemu ya utawala bora kwa hivyo wale ambao wanafanya hivyo nawalaani sana na kauli zao kama hizo.

Mhe. Mwenyekiti, Rais wetu tumeona kwamba anashaurika akipata ushauri ambao una tija ya nchi yetu tayari anaufuatilia, sio kila ushauri anauchukua lakini ule ambao kwamba anaona una mafanikio mazuri katika nchi yetu anautumia na tunaona jinsi gani alivyofanya kazi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nafarijika zaidi pale Rais wetu aliposhauriwa kuona kwamba ahadi zake alizoziweka anazitimiza hasa alipoahidi kutengeneza barabara ya Finya/Chimba tokea mwaka 2015 na sasa imepata kauli ya kwamba tayari barabara ile itaweza kushughulikiwa. Lakini namuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa anieleze hatua gani ambayo kwa sasa imefikia ukiachia ile ya mwaka 2016 iliyofika kwa kuwekwa pegi eneo lile. Je, fidia imeshalipwa na wao tayari wametangaza kwamba barabara hii itajengwa. Fidia zimeshalipwa na mkandarasi ameshapatikana na fedha je, zimeshakuwepo atakapokuja naomba anifahamishe.

Mhe. Mwenyekiti, *(Microphone iligoma hapa)……,* wananchi wa Fundo kuona kwamba wakati wanateremka vyombo kuelekea juu, aliahidi kwamba sehemu hii ataishughulikia. Sijui ofisi yake imejipanga vipi katika kuona kwamba ile kero ambayo na yeye aliiona wakati alipoteremka boti kuelekea juu kwenye ufunguzi wa umeme kule Fundo. Ningeomba atakapokuja Mhe. Waziri hapa tuone kwamba atatujibu kwa namna gani kama tayari utekelezaji au bado, lakini ni mkakati gani uliowekwa katika kutekeleza ahadi ile ya Rais wetu mpendwa.

Mhe. Mwenyekiti, ipo haja kuona kwamba sasa wale ambao kuwa wanabeza kuona kwamba Chama cha Mapinduzi walikihama kwa sababu hakina maendeleo, lakini Chama cha Mapinduzi kinateleza ahadi yake kama walivyoahidi kwenye kitabu chake na msimamizi wa haya ni Rais wetu. Kwa hivyo sioni sababu tena maendeleo ambayo yamejitokeza katika visiwa hivi kuona kwamba bado wanabaki upinzani.

Mhe. Mwenyekiti, mimi natoa wito kukaa upinzani bado ni tatizo kwa hivyo warudi wale wapinzani ambao kuwa wameingia kwa sababu hakuna maendeleo sasa warudi nyumbani CCM itawapokea na sababu hii inayowafanya hata wenzetu kule Tanzania Bara, ukawakuta wanaingia

makundi kwa makundi baada ya kumuona Rais wetu wa Jamhuri ya anavyotekeleza Ilani na kuona kwamba wananchi wanafaidika. Kwa hivyo wenzetu hata wale wa CUF karibuni sana CCM.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa taarifa nyengine ambazo kuwa ameweza kuzitoa jinsi ya uendeshaji wa serikali yake. Kwa mfano hivi sasa anavyosema kwamba wananchi wasiibugudhi serikali yao, wawatumie Wajumbe wao wa Baraza la Wawakilishi majimboni kupeleka kero zao na mimi naungana mkono na hilo, sisi tuko tayari kupokea maoni yao bila ya kujali wanatokea chama gani. Lengo letu ni kujenga nchi yetu, kwa hiyo njooni na *ZBC* nao wala *list* yao suala hili kila asubuhi, kwa hivyo ni vyema na sisi wananchi tukaitumia fursa hii, kwa kusema kweli Rais wetu anajitahidi sana.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika uchangiaji katika kitabu hii cha hotuba ukurasa 45 Programu ya Usimamizi wa Majukumu ya Kikatiba na Kisheria ya Baraza la Mapinduzi na Kamati ya Makatibu Wakuu. Mhe. Mwenyekiti, kitabu hichi ibara 112 kifungu kidogo namba 5, imesema kwamba kuimarisha tafswira ya hali ya utumishi umma nchini, hili ni jambo muhimu sana tumemuona Rais wetu amewajali sasa suala hili mimi nilitaka nijue kupitia ofisi hii. Je, baada ya Rais kuchukua juhudi ya kuongeza mishahara ya wafanyakazi ni tija gani iliyopatikana kwa serikali kuona kwamba wafanyakazi wanatenda kazi ipasavyo, isiwe wanaongezwa mishahara lakini bado kazi imedoroda, naomba atakapokuja katika tafswira hii ya utumishi iko hali gani.

Lakini vile vile kuhusiana kuimarisha uhusiano wa ushiriki katika jumuiya ya majukwaa kikanda ya kimataifa. Mhe. Mwenyekiti, hili jambo muhimu sana kwa sababu kadri ushirikiano unavyokuwa umoja tunaweza tukasaidiana katika nyanja mbali mbali, pamoja na kuratibu kazi za ziara ya Mhe. Waziri. Mhe. Rais katika kuona kwamba ana mpango mzuri uliooneshwa hapa kutayarisha mikutano kati ya Mhe. Rais na Wizara ya SMZ ili kutathmini utekelezaji wa mipango kazi na kufuatilia utekelezaji wa maagizo ya maelekezo yanayotolewa. Hili ni jambo muhimu sana Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo naomba niendelee kwani litaweza kuleta tija na wale watendaji kule mawizarani wanajiandaa kwamba kuna siku tutakaa tuulize tumetekeleza lipi na lipi hatujatekeleza. Hii itasaidia kuonesha kiwango zaidi cha utumishi katika utumishi wa umma katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo mimi nishukuru sana, mchango wangu ni mdogo lakini hayo maeneo niliyoyagusa naomba atakapokuja waziri anipe maelezo na mimi naunga mkono hoja hii 100 juu ya 100 bila ya kuondoa kitu. Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru sana Mhe. Shehe Hamad Mattar kwa mchango wako, Waheshimiwa Wajumbe kabla sijawaita Mawaziri na Manaibu Mawaziri ambao wameleta maombi wanataka kuchangia hotuba hii, basi tuna wachangiaji wetu watatu ambao ni wajumbe wa kwanza atafuata Mhe. Miraji Khamis Mussa na atafuatiwa na Mhe. Jaku Hashim Ayoub na Mhe. Maryam Thani ajiandae.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya kuchangia Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa 2018/2019 Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

La mwanzo Mhe. Mwenyekiti, naomba nichukuwe fursa hii adhimi kumshukuru Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa namna anavyotekeleza Ilani ya chama chetu kwa kiwango na asilimia kubwa sana kuona nafasi ya kumshukuru kwa hilo eneo, lakini jengine naomba nimshukuru Mhe. Waziri kaka yangu Issa Gavu, Katibu Mkuu, Mhe. Salum Maulid Kibanzi, kaka yangu vile vile, lakini ni Washauri wa Rais, wanaofanya kazi katika Ofisi hii, wasaidizi wa Katibu Mkuu na wenginewo wote, kwa namna bora ya mashirikiano yao ya kumsaidia Mhe. Rais kutekeleza majukumu yake vizuri.

Kwenye hili Mhe. Mwenyekiti, la leo mimi sina cha kuzuia kwa sababu asilimia 90 ya kitabu hichi, yale ambayo nilichangia bajeti iliyopita 2016/2017, 2017/2018 yamejitokeza utekelezaji wake karibu asilimia 95 naomba niwapongeze sana viongozi wote wa taasisi hii. Nilipokuwa nikipitia toka shukrani alizozianza Mhe. Waziri lakini mpaka kumalizia ule utekelezaji wa programu ziliomo ndani ya kitabu hichi, basi nimeona mambo mengi yametekeleza. Kwa hivyo nitakuwa na kazi ndogo sana ya kuchangia baadhi ya maeneo tu lakini kwa ujumla ningekuwa sina fadhila vizuri kama tulichangia hotuba yao lakini na wao wakenda wakayatekeleza mambo kama ambavyo na yale matarajio ya Waheshimiwa Wajumbe pamoja na mimi kwa asilimia hii waliyoileta ndani ya kitabu chao. Kwa hivyo na mimi nasema leo kama sikuchangia sijawatendea haki, kwa sababu wamefanya kazi kubwa na kila eneo nililolisema naona ziara ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, lakini ziara za Mawaziri na Tume zile za wataalamu zimeeleza vizuri kwenye maeneo mengi.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo, na maelekezo ambayo tuliwapa wenzetu naomba sasa nianze kuchangia kidogo tu. Juzi tu kama sikosei kwa sababu liliona tu tarehe 9 Mei kwenye TV sasa sijui kama ule uzinduzi ulifanyika tarehe 9 au sisi tulionesha 9 kwa sera ile ya *DIASPORA*, sasa. Mimi nimeona tarehe 9 kwenye TV, lakini wenzetu hawa sijui kama ndo tarehe 9 au tarehe ngapi walizindua lakini lengo langu kuzungumzia uzinduzi wa Sera ya *DIASPORA* niliichangia na ilikuwa karibu mara nyingi nauliza mpaka masuala ya ndani ya Baraza hili kuhusu sera ya *DIASPORA*, lakini juzi wenzetu wametimiza kile kilio ambacho hata na sisi tulikuwa tunajaribu kukichangia.

Kwa hivyo nimpongeze sana Mhe. Waziri, Katibu Mkuu na Viongozi wote walioshiriki kukamilisha Sera ya wana *DIASPORA*. Sasa niombe tu Mhe. Waziri sera ni jambo la mwanzo na naamini tunapopitisha sera tutakuwa tumepitisha na miongozo mingi katika utekelezaji wa ile sera, ikiwemo uwekezaji labda katika utaratibu wa wanzetu wale Wazanzibari wanaoishi nje ya nchi, lakini mashirikiano na taratibu zote tumewawekea mle. Kwa hivyo mimi sijawahi kuipitia hiyo sera lakini kwa utaratibu wangu nitakuja kukwambia angalau na mimi unipatie ili niweze kufaidika nao na nishauri vizuri kwenye eneo hili.

Mhe. Mwenyekiti, la pili katika Idara hii naomba twende sasa kwenye *data base* ya kuwatambua na kuwaelewa mahali walipo ili kuna siku tu serikali, kama ina haja ya wataalamu fulani kwenye eneo hili la Wazanzibari wanaoishi nje ya nchi, tuweze kuwapata kwa urahisi kwa sababu ni vijana wetu, ni watu wetu na wana uchungu wa nchi hii. Kwa ukweli kwenye jambo hii la *data base* ili kuweza kuwatambua na kuwajuwa mwahala walipo ni jambo la pili ambalo namuomba sana Mhe. Waziri na Katibu Mkuu, kwa sababu lile kubwa nishakamilika naamini na hili ni dogo

likaratibiwa vizuri maelezo yataenda vizuri, lakini na sisi tutafaidika kwa njia moja au nyengine kwa wenzetu hawa, Wazanzibari hawa ambao wanaishi nje.

Lakini suala la pili, ambalo pia niombe kwa Mhe. Waziri kwa sababu mambo yote yameenda vizuri leo nitakuwa namuomba tu, ukipitia sera hii, ukipitia uwepo wa wana *DIASPORA* lakini ukenda hasa katika dhima iliyonayo Idara hii ya Uhusiana na Nchi za Nje ambayo inaratibiwa na Ofisi ya Rais Ikulu, dhima kubwa ukiitizama na ile mikutano wanayokwenda kama ya *EAC, COMESA, SADC*, unakuta ina dhana kubwa ya kiuchumi ndani yake. Lakini sisi wengine tuna *a,b,c* kidogo, lakini naamini sehemu kubwa ya Wajumbe wa Baraza hili hawana *a,b,c* ya yale mafanikio makubwa yanayopatikana kwenye Idara hii ya Ushirikiano ya Kimataifa hasa kunako maeneo ya kuhudhuria mikutano ile ya ushirikiano wa kikanda na jumuiya zake mle.

Sasa nimuombe Mhe. Waziri kwa sababu tunajua eneo kubwa la dhana ya kiuchumi kwenye idara hii lipo pale, basi ukichanganya na sera ya wana *DIASPORA* kwa pamoja, angalau japo siku moja kwa kujenga uwelewa zaidi wa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, ili tupate kuchangia eneo hili basi iandaliwe japo semina ndogo tu ya kutujengea uwelewa zaidi, mimi nina *a,b,c* lakini nasema wenzangu kunako dhana nzima hii ya kukamilisha kuijua sera lakini pia kwenda kwenye utaratibu wa kuijua Idara ya Uhusiano na yale mambo yanayopatikana katika ushirikiano wa kikanda, basi tukilifanya hili tutalifanya jambo moja kubwa sana, lakini pia tutafanya Wajumbe hawa wa Baraza la Wawakilishi kunako eneo hili la ushirikiano wa kimataifa wajuwe tu, kuna eneo kubwa la uchumi ambao yale makubaliano yetu na wanajumuiya ambao tunakwenda nao kwenye mikutano mbali mbali na yale makubaliano yakitokea na zile fursa zinazotokea basi Wajumbe wa Baraza hili watapata kufaidika.

Sasa hili nikuombe sana Mhe. Waziri, Katibu Mkuu naamini yupo na ananisikia kwa kujenga uwelewa mzuri zaidi wa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu Mhe. Mwenyekiti, basi tulikuwa tunaomba watufikishe kwenye eneo hilo tutawashukuru sana. Lakini jengine nilichangia katika kikao kilichopita suala la kodi zile au *tariff* kwa lugha nyengine. Ufafanuzi wake kunako hichi kitabu kizima nimepitia sikuliona, labda katika mchanganuo wake maana linaweza kutokea hapa naweza kutokea Wizara ya Biashara, lakini kwa faida ya wafanya biashara wetu, maana kuna changamoto kubwa kunako eneo hili. Na tukifanikiwa kutatua changamoto zile kuna faida kubwa sana ambazo wanazipata wafanyabiashara wetu sasa tu maelezo. Mhe. Mwenyekiti, niseme kama maelezo hayapo pia ndo nishapitisha hotuba hii kwa asilimia mia moja, lakini tupate maelezo kwa faida tu ya wafanyabiashara wetu tuone kunako eneo hili basi changamoto zile zimetatuliwa kwa kiwango gani.

Lakini pia katika kitabu hichi wakati napitia kuna eneo moja Mhe. Mwenyekiti, nimuombe Mhe. Waziri namba 25, katika ukurasa wa 10 na namba 25, kuna maelezo tu chini mwisho ambayo Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi aliunda Kamati ya Kufuatilia, ambayo na hiyo Kamati pia ishawasilisha taarifa zake. Lakini kwa utaratibu na *nature* ya uzito wa kamati hii kama zile taarifa ziliishia kule, pia naomba usije ukanijibu kwa sababu nitakuwa sina adabu, lakini kama yale maelekezo na ufafanuzi umetoka kwa faida ya wananchi ambao tayari baada ya uundwaji wa kamati ni jambo jengine taarifa kuwasilishwa ni jambo la pili.

Lakini niseme tu kama utaratibu huu Mhe. Rais kashauri kwa faida ya wananchi wake basi eneo hili mambo gani ambayo yalitokea ili tupate na sisi kupata faida, lakini kama hajayatowa nakuomba sana Mhe. Waziri utakapokuja kujibu ukipita tu na kunyamaza kimya mimi nishajua kama tayari yale mambo hayajapata fursa ya kuzungumzwa tusubiri wakati ukifika tutayapata.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho naomba sana Wajumbe wa Baraza hili Tukufu kwa uzuri wa kitabu hichi, nilipokuwa namsikiliza Mhe. Hamza kwa umakini aliacha tano tu zile, alichangia kwa alisema anaikubali bajeti hii kwa asilimia 95 akabakisha 5, lakini nilikuwa nadhani 5 ile iliyobakia labda kwa rangi ya hichi kitabu. Sasa kwa mara nyengine Mhe. Waziri hichi kitabu kibadilishe rangi kiwe chekundu hii bajeti ipite kwa asilimia 100.

Baada ya hayo naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia 100 nakushukuruni sana viongozi wa taasisi hii pamoja na wewe mwenyewe.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana nakushukuru Mhe. Miraji kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Jaku Hashim Ayoub atafuatiwa na Mhe. Maryam Thani na Mhe. Waziri Asiye na Wizara Maalum Mhe. Said Soud ajiandae.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kukushukuru kunipa fursa hii na *actual* ndio kwanza nifike nikitokea Dodoma kwa kuwasilisha wananchi na Wazanzibari kwa jumla.

Mheshimiwa nichukuwe fursa hii kwanza kabla ya yote kumshukuru Mwenyezi Mungu kuweza kunisimamisha hapa, kwa kuweza kupumua na kuvuta pumzi zake alizoniazima ambapo sijui sasa ngapi atazihitaji, hii ni neema kubwa wala si ujanja wangu wala akili yangu ni maarifa yangu, hii ni neema kubwa na baada ya siasa kuna maisha nje.

Mhe. Mwenyekiti, niendelee kuwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Paje kwa kuniamini na mimi nitajitahidi kwa hali na mali kama iwezekanavyo kuwatumikia au kuwasemea kero zao walizonituma, kuja kuwasemea na kama unavyojua cheo ni dhamana siku ya siku tutakuja kuulizwa je! Tumetumia vipi vyeo vyetu hivi, ee Mheshimiwa nitakuwa sijafanya haki wananchi wangu pamoja na Wazanzibari wote wa Unguja na Pemba waliopata maafa ya mvua hizi na upepo mkali ukiwemo Michamvi, Paje na Bwejuu na shakusikitisha pana Ofisi ya Mfuko ambayo inasimamiwa na Makamu wa Pili wa Rais, sikuiona kufika Paje, Michamvi na Bwejuu ni sababu gani. Jambo lililonisikitisha sana na limeniuma sana wala sina nia ya kutaka kugombanisha na Serikali na wananchi wangu lakini jambo limenisikitisha kuna mfuko wa bajeti hata kufika kule kutowa salamu basi jambo limenisikitisha kweli kweli.

Wananchi wangu wamepata hasara kubwa mapaa yao ya nyumba yameizuka, kuna hospitali kule haipo sasa hivi Michamvi, wanatibiwa wananchi kwenye nyumba ya mtu, kitu cha kusikitisha sana. Mhe. Makamu wa Pili Mhe. Mohamed Aboud, Naibu wa Waziri wa Wizara hiyo mngefanya siku na kule kunako ngome ya Chama cha Mapinduzi kwa kusema kweli.

Mhe. Mwenyekiti, nitakuwa sijatenda haki kama sikumshukuru Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein, kwa jinsi anavyotumikia

wananchi wa visiwa viwili hivi vya Unguja na Pemba, bila ya kujadi itikadi ya chama, rangi wala kabila na kwa kuitekeleza vyema Ilani ya Chama cha Mapinduzi hivi juzi tu, tumemuona tu nafikiri kamaliza ziara za Unguja na Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, na amejitahi kabisa kwa hali na mali Ilani ya Chama cha Mapinduzi kuitangaza vengine, ni vizuri kabisa alikutana na mabalozi katika wizara hizo akifanya kazi kubwa. Mheshimiwa niwape pole wale waliotegemea kupata Uwaziri na Unaibu Waziri kwa bahati mbaya hawakupata hivi juzi, niwambie tu wasiwe mbali pengine kutakuwa na mabadiliko pengine huko mbele wanaweza wakapata. Nitakuwa sijamfanyia haki Mhe. Waziri Mhe. Issa Ussi Haji Gavu na pamoja na timu yake yote kwa pamoja. Na vile vile, nimpongeze kwa kitendo kizito alichokifanya jana katika jimbo lake ambao ni historia kwa Zanzibar haijawahi kutokea, katika kukumbuka mwana siasa alifanya mambo mazito sana katika Wawakilishi jana, alichafua hali ya hewa jimboni Chwaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa ushauri wangu au pendekezo langu narudia tena, ushauri au pendekezo langu wizara zote zinapofika wakati kama huu wa kupitisha bajeti katika hivi vitabu wangeandikwa yaliyofanywa na Mhe. Rais, kama Wizara ya Afya, Wizara ya Ardhi, wizara ya maji angalau kukumbuka hichi chombo ndio cha wananchi, wananchi ndio chombo hichi wanachokisikiliza. Mhe. Rais huyu kafanya mengi na mengine wananchi hawayajui, chombo hichi cha wananchi ndicho wanachokisikiliza.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitazungumza baadhi ya mambo muhimu au makubwa, ingawa muda hautotosha kuyataja yote aliyoyafanya Mhe. Rais. Nilikuwa nikisema mimi hata nikiamshwa saa 9:00 za usiku au saa 10:00 nina usingizi mkali pale nikiulizwa Mhe. Raisi kafanya nini, nitasema bila ya kigugumizi nitasema kawatumikia wananchi katika mambo muhimu ya Sekta ya Jamii hasa katika Sekta ya Afya, kuna Wizara ya Elimu kafanya mambo mazito, hata wengine ma-Rais wameiga kutoka kwa Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, sina nina kama nataka kujipendekeza kwa Mhe. Rais kwamba nataka Uwaziri au Unaibu Waziri hapana na maneno husema mimi, moja ni moja na kama mbichi ni mbichi na kama kavu ni kavu, husema ukweli na msema ukweli ni mpenzi wa Mwenyezi Mungu.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, katika Sekta ya Afya tulikuwa hatuna *ICU* hapa Mnazi Mmoja, niliwahi kusema tuna gereji na anayeingia hatoki mle mpaka Mwenyezi Mungu apitishe rehema zake tu. Imejengwa *ICU* hatukutegemea hapa, alifika Waziri kutaka kujiuzulu Mhe. Juma Duni humu ndani Baraza lililopita, sasa hivi *ICU* ya kileo katika Sekta ya Afya.

Mhe. Mwenyekiti, akina mama walikuwa wanapata shida wakati wa kujifungua mpaka aweke Sh. 40.000/- Mnazi Mmoja, lakini kwa umakini wa Mhe. Rais ada zote kaziondoa. Kuna watu wanatoka Bara wanakuja kujifungua huku, tuzitaje neema zake hizi. Sisi sote tunategemea bajeti inayokuja Wizara ya Afya imeongezwa pesa hasa katika Sekta ya Madawa harufu niliyoisikia, zimeongezwa pesa kutoka 1.5 bilioni mpaka 5.3 kwa mwaka huu, sio jambo la mchezo, apongezwe Mhe. Rais, kwa kazi nzito anayoifanya jinsi anavyojali wananchi. Hiyo ni harufu niliyoisikia inaweza ikawa pengine ikageuka lakini ni harufu tutasubiri itakapofika tuiyone. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, kujengwa kwa majengo mawili mapya kwa Hospitali ya Mnazi Moja, siyo jambo dogo. Jengo moja la mama, la pili la mama na mtoto, ni neema kubwa. Katika hiyo Sekta ya Afya kuna mashine ya *NRI* ilikuwa hatuna Mnazi Mmoja, mashine ya kileo na ya kisasa, vipimo ni ghali *CT Scan* ni laki mbili mpaka laki mbili na nusu mpaka laki moja na nusu, leo hapa ni bure hii ni neema kubwa.

Mhe. Mwenyekiti, kama jengo la Hospitali ya Mkoani hakuna mtu aliyetegemea ni neema kubwa, jengo la kileo, kuna zana ambazo hata madaktari wanashindwa kuzitumia ni jengo la kisasa kabisa la Abdalla Mzee Hospitali. Juzi kuna mashine za *X-ray* mbili mpya zimeletwa Mnazi Mmoja nafikiri zinaendelea kufungwa nilikuwa nikipiga kelele sana humu ndani, hapana *X-ray*, lakini kelele au hoi hoi nacho kilindo, ndiyo hichi ambacho kinasaidia. Mawaziri tunapochangia msituone kama wabaya humu ndani, hizi hoi hoi ni kilindo kinachosaidia, Sekta ya Afya imeinuka. Msifike pahali hata hiyo bajeti mnayoiona kutoka milioni 7 mpaka milioni 12.7 siyo jambo la mchezo kwenye Wizara ya Afya, msifikiri Mawaziri watu hawakuoneni moja ya majukumu yetu, kuisemea serikali na kuihoji.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, nilisema mimi Hospitali ya Mnazi Mmoja haiwezi kufika kuwa ni hospitali ya Rufaa, kuna mambo hayapatikani, wagonjwa wa macho wanakwenda Kwamtipura kule Mikunguni, leo jengo lile pale linaendelea vizuri ujenzi, ile ndiyo maana ya Rufaa. Huwezi kwenda pale baadae ukenda huku, ile siyo Rufaa. Rufaa maana yake vitu vyote vinapatikana pale.

Mhe. Mwenyekiti, kuna jambo jengine la *mental*, sasa hivi kunajengwa wodi sasa hivi ya vitanda 100 kulikuwa kumeoza *mental*, ujenzi unaendelea.

Mhe. Mwenyekiti, niendelee na Hospitali ya Makunduchi na Kivunge kupandishawa kuwa Hospitali ya Wilaya ni jambo zuri. Jengine Ofisi ya Mkemia Mkuu Maruhubi ni ya kileo na ya kisasa imejengwa majuzi tu. Kuna harufu nyengine ya *DNA*. Waheshimiwa humu sote tulikuwa tunapiga kelele humu ndani kuhusu *DNA* jambo la DNA, lakini kuna harufu hiyo, siyo muda mrefu Mwenyezi Mungu akipenda. Nani aliyefanya mambo haya. Chini ya uongozi wa Rais aliyemakini. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, Bodi ya Chakula imepanda hadhi sasa hivi, inatambulika kutokana na vipimo sasa hivi na ipo Wizara ya Afya hii. Juzi ndugu zetu wa Wapemba, yupo wapi…., akaja akahamaki, wamepelekewa madaktari na wauguzi kwa wingi juzi tu hivi, wakafanye kazi kuwatumikia wananchi bila ya kujali itikadi ya siasa ni mambo ya uongozi. Hapo niliposema uongozi itafika pahali tutakwenda kuuliza, uongozi ni dhamana.(*Makofi*).

Niombe sijui kama washauri wa Rais wapo hapa, hili nafikiri mwenyewe Bwana Mkubwa anatizama, kama wapo juu naomba hili kidogo walipeleke kama ombi kuhusu Bohari Kuu kutaka kujengwa Pemba. Nipendekeze au ni ombi Bohari Kuu inahitajika Pemba ya kuhifadhi madawa, *formula* hii ya kupeleka dawa Pemba siyo nzuri kwa muda huu. Ninafikiri Mhe. Rais hashindwi hili kwa umakini wake, mengi tunayazungumza hapa. Katika mtu niliyepiga kelele au niliyochangia kwa asilimia 80 katika sekta ya afya nimefanikiwa mimi kwa Mhe. Rais.

Nimshukuru na hili ni ombi Washauri nakutumeni, *formula* inayopeleka dawa pemba haiko vizuri, kujengwe bohari kuu.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Afya kuna mengi, siwezi kuyamaliza, niguse kidogo na Wizara ya Elimu. Jambo kubwa kufuta ada na michango Mhe. Rais kutoka darasa la kwanza mpaka darasa la saba kaondoa. Marais wengine wameiga utawala kutoka kwa Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein, si jambo dogo ni jambo kubwa. Kama hapa hapatoshi, bajeti tutakayoipitisha keshokubwa Mwenyezi Mungu akitujaalia mwezi wa saba mtasikia miujiza mengine Mwenyezi Mungu akipenda, si vizuri kusema tukishakupitisha bajeti mtasikia. Nani kafanya haya, yamefanywa chini ya uongozi wa Rais Makini. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, ndio pale ninapokuombeni Mawaziri msaidieni Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein, ndiyo yale moja moja, mbili mbili, kuna fununu huko mpaka Elimu ya Sekondari huenda ikaondoshwa. Elimu ya Juu wanafunzi wanafanya vizuri karibu 20 serikali inaji-*commit* ada, posho inawalipia, hii ni neema kubwa. Vyuo Vikuu vya Zanzibar sasa hivi vina hadhi na vinatambulikana. Skuli zimejengwa tena za ghorofa na za kileo itabiti hapa kidogo nizinukuu maana ni nyingi tu.

1. Skuli ya Rahaleo maarufu inaitwa Skuli ya Mwembeshauri
2. Skuli ya Bububu
3. Skuli ya Kinuni
4. Skuli ya Chumbuni
5. Skuli ya Fuoni hizi zote ninazozitaja ni za ghorofa.
6. Skuli ya Fuoni Pangawe,
7. Skuli ya Kwarara ya Mhe. Ali Suleiman Ali, skuli hii ina sifa mbili, kuna Chuo mle ndani cha TV na redio, zote shughuli za nani hizi? Eeh!
8. Skuli ya Kiduteni lilikuwa gofu limekaa tu sasa hivi linaendelea

Mhe. Mwenyekiti, tuje kwa upande wa Pemba.

1. Skuli ya Kizimbani
2. Skuli ya Wete
3. Skuli ya Wara hii ipo Chake Chake
4. Skuli ya Micheweni
5. Skuli ya Wambaa ipo Mkoani
6. Skuli ya Jumapindua ipo Mkanyageni

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa una dakika tano.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, haya mambo yamefanywa na Mhe. Rais, kuna Skuli ya Donge inaendelea vizuri sasa hivi skuli kubwa ile.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye sekta ya maji, maana yake itabidi huku nikatize. Kwanza nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Rais kwa uteuzi aliyoufanya kwa Mkurugenzi yule anaitwa Mussa Ramadhan Haji, kama hivi. Yule kijana kateuliwa juzi tu sijui kama miezi minne imefika, mabadiliko tumeyaona muda mfupi tu kuteuliwa kwake. Kuna maeneo sugu yalikuwa hayapati

maji au hayapo vizuri, kama nitakosea Waheshimiwa Wajumbe naomba mnisamehe, mimi sio mkamilifu.

1. Muungano kulikuwa hakupo vizuri
2. Jang'ombe kulikuwa hakupo vuziri
3. Matarumbeta kulikuwa hakupo vizuri
4. Sogea Sebleni
5. Mtoni
6. Shaurimoyo

Mhe. Mwenyekiti, kwa taarifa nilizokuwa nazo kunaendelea vizuri sio kama kupo 100% hapana, lakini kupata kidogo sio kama kukosa, amejitahidi. Kuna harufu nyengine huko kwamba kuna mpango wa miji 17 milioni 33 dola kupitia Serikali ya Tanzania Mradi wa Wahindi *Exim Bank* kwa tatizo la maji nafikiri kabla ya kuondoka Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein litakaa sawa ninavyoamini mimi. Vile vile katika bajeti inayokuja nitakuwa sijamfanyia haki Mhe. Rais kuna harufu ninayoisikia nayo kuwa Michamvi na wao tokea dunia ilipoanza huwenda wakafaidika na mradi huo.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, nije kunakokitabu hiki ukurasa wa 10 Kiwanda cha Sukari Mahonda. Kama kuna watu waliofanya kazi hawa Kiwanda cha Sukari Mahonda wale wamefufua maiti. Leo sukari yao kupelekwa Bara imekuwa kigugumizi. Leo bia inatoka Bara kuja Zanzibar hapa, saruji inakuja Zanzibar, nondo inatoka huko kuja Zanzibar, ndio maana tukasema huu muungano aah! maana sifahamu kama unalinda viwanda vya Tanzania Bara, mimi nimewauliza juzi Dodoma ikawa vurugu na hata kuchangia yangu Dodoma imekuwa kipingamizi sasa hivi, mpaka nikitaka kuzungumza naulizwa unataka kuzungumza kitu gani, imekuwa kazi.

Huu Muungano hata Mhe. Rais wetu alisema alivyofungua jengo la Mtakwimu kimo humu, linalofanywa Bara na Zanzibar lifanyike, ikiwemo Tanzania Bara ikiwa Zanzibar. Leo bidhaa hapa kupelekwa Mhe. Hamza Hassan Juma kapiga kelele sana hapa mpaka madaa mwisho. Huu Muungano sio lugha ya Kiarabu ukavutia kwako tu. Kiarabu ukiandika unavutia kwako tu. Viongozi wetu wanaoingia katika Muungano siku zote mnatwambia mnatatua kero, hatuzioni, mnatwambia kero tatu, juzi niliwaambia mimi hizi kero tatu ziko wapi, *ICU*.

Mhe. Mwenyekiti, mpaka Mhe. Mohammed Aboud Mohammed kwenye magazeti anasema bado kero tatu, tunayo magazeti ya Zanzibar Leo, mpaka leo. Muungano usiwe wa upande mmoja tu, wateteeni wananchi. Mimi kule nasokotwa kupita kiasi kwa kuyatetea maslahi ya Zanzibar. Leo sukari ile kuipeleka kule kuna tatizo gani, sukari inatoka Zambia inaingia pale. Ndiyo niliyoyasema maji yanayotoka Zanzibar kwenda Tanzania Bara kwa ndugu zetu wa damu imekuwa kigugumizi. Si haki na wala sio halali, tuletewe bia hapa, saruji tuletewe, maji watuletee, sisi kupeleka bidhaa yetu kule inakuwa shida. Mhe. Mwenyekiti, mpaka Mawaziri wanahamaki kule Bungeni sasa hivi, nikiinuka tu ninakuwa kama damu ya kunguni ni mtihani. Tuangalie kote kote ndio maana ya kuungana, niliwauliza mimi *what is union?* Nipeni *definition* ya muungano. Muungano ni watu kushirikiana ulinzi, ajira na mambo mengine, ndiyo maana ya muungano. Lakini inafika pahali mali ya Zambia, Uganda, Burundi, Kenya, hata juzi mafuta

yanayokwenda Burundi, Zambia na Congo, dola tatu wanatozwa Bandarini pale *Wharfage,* sisi dola 10. Tujiulize Mawaziri mnaokwenda kwenye Muungano.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti: Naomba umalizie Mheshimiwa muda wako umekwisha.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, nimalizie kwa Uwanja wa mpira wa Kitogani jimboni kwangu. Nimpongeze sana Mhe. Rais kwa jitihada alizochukua kwa kiwanja kile na anasema hata mwisho kama hakitokuwa majani muwafaka akatia majani ya bandia. Lakini kwa kumalizia hapa nitakera watu kidogo kama watakereka wanisamehe.

Wale wanaotaka kuvaa viatu vya Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein wakati bado, kama ikiwa wamo humu au wako nje, wampe Rais muda, tusije tukapanga makundi, tumpe nafasi. Viatu vile vinaweza vikawabana baadae, kama wamo ndani kama wapo nje, wampe muda Mhe. Rais wa wakati bado, wajitathimini kwanza uwezo wao kweli wanaweza kuvaa viatu hivi. Hata na Wawakilishi kumbe wamo humu nnatetewa, kwa hivyo tujitathmini tunaweza kuvaa viatu vya Mhe. Rais yule kweli na Uwakilishi na Ubunge na Udiwani. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru naona muda umekwisha.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Jaku Hashim Ayoub, nakushukuru kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Maryam Thani Juma atafuatiwa na Mhe. Waziri Said Soud na Mhe. Naibu Waziri wa Habari na Mambo ya Kale.

Mhe. Mariyam Juma Thani: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia machache katika hotuba hii ya Waziri wa Nchi, Afiri ya Rais na Mwenyekiti, wa Baraza la Mapinduzi.

Kwanza kabisa napenda kumpongeza Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake kwa ripoti hii ambayo ametuletea ndani ya Baraza letu tukufu, ripoti ambayo ina mambo mengi mazuri ambayo Mhe. Rais ameweza kuyatekeleza katika kipindi hichi cha uongozi wake. Mhe. Mwenyekiti, niseme mambo mengi ambao ameyanadi katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi, Mhe. Rais ameyatekeleza na yale ambayo kwa sasa tumeona anayafanya zikiwemo ziara mbali mbali anazozifanya kwenye nchi yetu na nje ya nchi yetu. (*Makofi*)

Niende katika ukurasa huu wa 8 kifungu cha 22 ambacho Mhe. Rais ametembelea Falme za Kiarabu. Falme hizi ambazo ni ushirikiano baina ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Zanzibar. Kwa kweli niseme Mhe. Rais kafanya jambo zuri hata leo hapa tumetangaziwa kwamba wamekuja wageni wetu kusaini kitabu cha kutengenezewa nyumba yetu ya makumbusho ya Beit-el-Ajaib.

Vile vile kwenye ukurasa wa 8 kifungu cha 24 imeeleza miradi mengine aliyotembelea ni shamba la kisasa la ufugaji. Ukiangalia na mimi kwenye jimbo langu kwa sasa kunataka kuanzishwa shamba hili la ufugaji. Kwa vile Mhe. Rais ameona ipo haja na sisi kuweza kupata mambo kama haya. Niipongeze sana na sisi tunaweza kupata faraja kwenye jimbo la Gando

tukapata shamba hili la ufugaji wa ng'ombe wa maziwa wa kisasa na sisi tupate kuneemeka katika mambo mbali mbali zikiwemo ziara alizokwenda kutembelea Mhe. Rais.

Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze sana Mhe. Rais kwa mambo mengi tu aliyoyafanya yakiwemo pencheni ya wazee. Hili ni jambo muhimu sana kwa nchi yetu ambapo baadhi ya nchi nyingi hatujaona jambo hili kulifanyika ni Mhe. Rais wa Zanzibar Dkt. Ali Mohamed Shein. Yeye ndiye aliyethubutu kuona wazazi wetu wana umuhimu wa kupewa pencheni hii. Nimpongeze sana na Mwenyezi Mungu amuweke kwa mambo mengi ambayo anatufanyia.(*Makofi*)

Vile vile napenda sana kumpongeza kwa dhati kwa kuona upo umuhimu kwa Kisiwa hichi cha Fundo kupelekewa umeme na wananchi wale ilikuwa kipindi cha muda mrefu hawana umeme, lakini Mhe. Rais katika ilani yake amenadi kwamba atahakikisha kwenye uwongozi wake Kisiwa cha Fundo kimepatiwa umeme na kwa sasa umeme huu tayari upo na wananchi wameufurahia mbali na Mhe. Rais hakujali kwamba wananchi wale wapo upande gani. Vile vile Mhe. Rais aliahidi kututengenezea maskuli yetu ya kisasa na mimi ikiwemo katika jimbo langu Skuli ya Kizimbani na kwa sasa tayari inaanza ujenzi huu wa Skuli ya ghorofa na ujenzi, nimekwenda kuuona unaendelea vizuri, nampongeza sana Mhe. Rais na wananchi wanamkubali Rais wetu kuona kwamba anaweza kutufanya mazuri kwenye kipindi chake.(*Makofi*)

Vile vile nielekee kwenye vituo vyetu vya afya anajitahidi na mimi nikiwemo kituo changu cha Junguni amekuja kukifungua kupitia watu wetu na misaada yetu ya hawa watu wetu wa *TASAF* na kituo kile cha afya kipo Junguni Mhe. Rais kakizindua na kina huduma nzuri, vifaa vizuri vilivyopo katika hospitali ile na kwa sasa wananchi wetu wanapata huduma bila ya kuwa hawafuati huduma katika hospitali kubwa ya Wete, wanapata huduma pale pale katika kituo cha afya cha Junguni.

Mhe. Mwenyekiti, na mimi napenda kumpongeza Mhe. Rais kwa dhati kwa mara nyengine tena kwa kututengezea barabara nzuri yenye sifa, yenye hadhi barabara yetu ya Wete Gando na barabara ya Wete Konde. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Rais anajitahidi kuelekeza watendaji wake kuwelekeza mambo mbali mbali lakini niseme baadhi ya watendaji. Mhe. Rais wanamuangusha na nasema hivyo kwa sababu katika kutembelea wananchi wake wa Gando Mhe. Rais alisema wale ambao hawajamaliziwa kulipwa fidia zao katika barabara ile ya Gando. Alipozungumza na wananchi aliahidi kwa watendaji kwamba waliobakia kuwa hawajalipwa fidia zao walipwe kwa haraka sana. Lakini Mhe. Waziri hili naomba kwanza ulijue Mhe. Rais aliwaambia watendaji wake hawa waliobakiwa kuwa hawajalipwa fidia zao muda mfupi huu ujao walipwe fidia zao wananchi waliobakia. Tukiangalia kipindi hichi ni kipindi cha mvua wananchi wale waliobaki hawajalipwa fidia zao wako kwenye vibanda vya mgongo, mvua inawanyeshea na Mhe. Rais aliahidi watu hawa wamaliziwe. Lakini bado watendaji wanasuasua, kwa nini watendaji wanasuasua kwa nini na Mhe. Rais kishaahidi walipwe wale.

Mhe. Waziri nakuomba hili ulishughulikie kwa moyo wako wote kwa sababu wananchi hawa wanahangaika na mvua inawanyeshea na kwa ushahidi nataka wende Gando uwaone wako kwenye vibanda vya mgongo na Mhe. Rais alizungumza nao ana kwa ana wananchi hawa wakamwambia matatizo yao na yeye akayapokea na Mhe. Rais ni mtendaji mzuri na ahadi zake anazoziahidi yeye anazitekeleza. Lakini watendaji wake wanamuangusha. Nakuomba Mhe.

Waziri kwa heshima na taadhima nakuomba hili ulishughulikie ili wananchi wale nao wapate makaazi mazuri kama wenzawao waliolipwa fidia kwa athari iliyotokea katika barabara ile ya Wete - Gando.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo ambayo nimechangia naomba niunge mkono asilimia mia moja kwa vile Mhe. Rais ameyafanya mengi katika nchi yetu naunga mkono asilimia mia moja hotuba hii. Ahsante. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Maryam Thani Juma kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum Mhe. Said Soud Said atafuatiwa na Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale na Mhe. Rashid Ali Juma Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi.

Mhe. Said Soud Said: (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum): Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kunipa nafasi na mimi kuchangia Ofisi hii, kwani hii ndio afisi yetu na kwa namna ambavyo inafanya kazi zake vizuri basi sina budi na mimi nitoe mchango wangu Mhe. Mwenyekiti kwanza nachukua nafasi kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ambaye hii ndio afisi yake hasa na afisi hii kwa kweli inafanyakazi za Wazanzibari wote bila ya kujali rangi, kabila, Dini wala kanda ya sehemu husika.

Mhe. Mwenyekiti, mambo mengi yameelezwa katika kitabu hiki lakini mimi nataka nitoke nje ya kitabu hiki nieleze yale ambayo hayakutiwa kwa sababu tungesema yaingizwe yote yanayofanywa na afisi hii basi haya mabuku mawili niliyoweka hapa yangekuwa madogo, yaani hii *valume I* na *volume II* yote yangekushanywa pamoja yote yote yangekuwa kidogo kutokana na utandaji unaotendwa na Ofisi hii kupitia Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ambaye ndiye Rais wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Baraza la Mapinduzi ndiyo roho ya Serikali ya Zanzibar na imejitahidi kwa kiasi kikubwa kuonesha uwezo wake kwa Wazanzibari katika kuwatengenezea yale yote yalioahidiwa kupitia Ilani hii ya uchaguzi ya mwaka 2015-2020. Afisi hii haikurupuki tu kufanya mambo bali hufanya mambo kwa utaratibu uliokubaliwa na chama kilichotawala yaani Chama cha Mapinduzi.(*Makofi*)

Hata hivyo napenda kuchukua nafasi hii kuwaeleza wale ambao kwa namna moja au nyengine hubeza maendeleo ya Zanzibar. Mimi sisemi kama hawa hawana macho, hawa wana macho wanaona lakini ni walevi wa madaraka, na ukishakuwa mlevi wa madaraka basi unataka mambo yote katika nchi uyafanye wewe na ikiwa uko katika nyumba una madaraka ya nyumba basi mle ndani ya nyumba unataka ufanye wewe, una madaraka ya taasisi ile taasisi unataka ufanye wewe. Sasa huu ni ulevi wa madaraka na unaosababisha mtu kuweza kusema hakuna kitu kilichoweza kufanywa. Mimi nasema ni vizuri watu wa namna hii wakaondokana na hii dhana ya ulevi huu ili wakaweza kuungana na Wazanzibari wenzao tukajenga nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar ni sawa na sehemu nyengine yoyote duniani kama tunavyoona maendeleo yaliyofika katika nchi za watu mbali mbali yamejengwa na wenyewe, na sisi Wazanzibari ipo haja kushirikiana kwa dhati kabisa kuleta maendeleo ambayo ndiyo

yatakayowafanya Wazanzibari kupiga hatua. Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar sasa hivi inaongozwa na Wazanzibari wenyewe kinda kindaki. Sasa akitoke Mzanzibari pembeni akaanza kuleta maneno ya kuwabagua Wazanzibari na kuwagawa makundi kwa makundi, Mzanzibari huyu lazima aepukwe na watu wamkimbie kwa maana hana nia nzuri kwa Wazanzibari.

Afisi ya Baraza la Mapinduzi tukisema kwamba tujadili kwa urefu ni kama nilivyosema hatumalizi. Lakini kwa uchache tu nataka niseme Rais wa Zanzibari na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi anawajali wazee walio hai na hata waliokufa. Walio hai anawapa shilingi elfu ishirini ishirini na waliokufa wale kina Siti bint Saad amewajenga nyumba ya kumbukumbu ili wakumbukwe mpaka dunia imalize, watu wawe wanakumbuka na kila mtu muhimu ataekwa kule ili kwa ajili ya watu waweze kuwakumbuka watu hawa. Kwa maana hiyo ni kwamba Dkt. Ali Mohamed Shein ni Rais mtendaji ambaye kwa namna mmoja au nyengine huwa anataka awatendee Wazanzibari haki ya Mapinduzi yao ya Zanzibar.

Mhe. Rais ameweza kuzingatia matatizo ya Zanzibar juu ya hoja nzima ya kukidhi maisha na kuboresha maisha, amepandisha mishahara kwa asilimia mia hakuna mtu ambaye anaweza kupandisha mishahara kwa asilimia mia zaidi ya Dkt. Ali Mohamed Shein katika Afrika hii hakuna na nasema hivyo kwa uhakika kabisa. Lakini yeye ameweza kuwapandishia Wazanzibari mishahara ya asilimia mia bila ya kujadi kabila zao rangi zao, Dini zao, taasisi zao au watu wanapotoka. Na hoja hii anayoifanya Dkt. Ali Mohamed Shein amekuwa akifanya kwa Unguja na Pemba bila ya kuchagua, ameweza kuboresha elimu ambayo sasa Zanzibar ina Vyuo Vikuu, ameweza kuboresha afya ambayo sasa Zanzibar ina madaktari bingwa wazuri, wazaliwa, wazalendo na hospitali za kisasa. Kwa mfano kama hivi karibuni Mhe. Mwenyekiti, nilifika Hospitali ya Abdalla Mzee. Hospitali ya Abdalla Mzee ina zana za kisasa ambazo kwa Tanzania ni sehemu ya pili ni Hospitali ya pili kwa Tanzania nzima yenye uwezo wa zana namna hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, pale Abdalla Mzee nilionyeshwa mashine ambayo Wazanzibari napenda hasa wasikie kwa dhati yenye uwezo wa kupima *HIV* kwa dakika tano tu, unataka kwenda kufunga ndoa huna haja ya kukaa miezi mitatu mnachukuana kama mnakwenda kwa Kadhi, kama mnakwenda kwa Mawalii basi mnapita pale mnapima mnakwenda zenu kufunga ndoa bila ya wasi wasi. Mashine ya kisasa ambayo ni ya aina yake. Haya yote yamefanywa na utekelezaji wa Ofisi hii. Ofisi hii inajali sana maisha ya Wazanzibari kwa kuboresha kilimo. Kilimo sasa hivi Zanzibar kimebeba ile nafasi ya kuwa uti wa mgongo. Wakulima wengi wanapatiwa zana za kisasa, dawa, mbolea na mambo mengine yote ambayo Mhe. Rais anayaagiza kila siku mambo kama haya yafanyike.

Tukienda kwenye hoja ya umeme kama walivyosema wenzangu umeme umeenea katika visiwa vidogo vidogo na hata vile ambavyo havijapata umeme basi bila ya kufika 2020 navyo vyote vitakuwa vimeshapata umeme. Tukienda kwenye suala zima Mheshimiwa la barabara, barabara zimejengwa bila ya kujali kwamba hapa pana watu kidogo hapa pana watu wengi. Kwa mfano kama watu wengi wamesema Ngomeni mimi niliuliza ile *quantity* ya watu waliopo pale, hata mia tatu hawafiki, lakini *everything* kipo pale, umeme upo pale, hospitali ipo pale soko la karafuu kubwa liko pale na maji safi na salama yapo pale na barabara ya lami ambayo ni ya kisasa kabisa una teleza tu moja kwa moja ni maendeleo haya. Na haya yote yanasimamiwa na

ofisi ya Baraza la Mapinduzi, kwa vile huyu Mhe. Rais tunaweza tukasema kwamba ni Rais mtendaji mwenye nia na dhamira za kuifanya Zanzibar ibadilike.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nikwambie kwamba Zanzibar inabadilika siku hadi siku kutokana na ahadi zake huyu bwana na kutekeleza vyema ilani ya uchaguzi tuangalie mji wa Fumba. Mhe. Mwenyekiti, mji wa Fumba utafikiri Ulaya ndogo na yale yote yametekelezwa kupitia uongozi bora wa Mhe. Rais kwenye Ofisi yake na usimamiaji wake wa mambo ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, tukitoka hapo kwenye suala Fumba tuangalie zaidi kwenye suala zima la mabadiliko ya mji wa Kwahani ambayo Rais anayapigia kelele saa zote kwamba lazima tubadilishe mji wetu na tuulete wa kisasa. Haya yatatendwa na sio muda mrefu na hoja hii hii ya Kwahani Mhe. Rais tayari anaelekeza na Kisiwani Pemba yafanyike vile vile mabadiliko kama haya.

Tukienda katika hoja nzima ya Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Rais amekuwa ni mtu ambaye kwa namna moja au nyengine anapenda kuboresha maisha ya Wazanzibar katika mazingira mbali mbali. Tuangalie leo Mbweni kuna majumwa makubwa ya kifahari ambayo yameibuka tu kama uyoga kutokana na maendeleo mazuri ambayo yanasimamiwa na Ofisi hii, tuangalie sasa hivi hoja nzima ambayo ina angaliwa ya utalii. Mhe. Rais anasimamia hoja za utalii katika nchi yetu sasa limekuwa ndio zao la uchumi ndani ya Zanzibar nzima hii Unguja na Pemba, bila ya kujali kwamba labda utalii ufanyike sehemu moja sehemu ya pili usifanyike. Sasa hivi anapiga kelele za kila namna utalii uimarishwe Pemba ili watu na wao waweze kujikwamua kiuchumi.

Leo hii Mhe. Mwenyekiti, kimsingi ni kwamba maendeleo yanayosimamiwa na Ofisi ya Baraza la Mapinduzi Zanzibar ni maendeleo ya kupigiwa mfano na ni maendeleo ambayo yanatija kwa Wazanzibari na ni vyema Wazanzibari wakawa tayari kudumisha, Mapinduzi ya mwaka 1964, katika hali ya kuilinda Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ili kuwa ndani ya mikono ya Wazanzibari wenyewe.

Nachukua nafasi pia ndugu Mwenyekiti kukwambia kwamba Ofisi ya Baraza la Mapinduzi linasimama kwa jitihada zote na juhudi zote katika kulinda Muungano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuwafanya Watanzania kuwa kitu kimoja na kuifanya Zanzibar kuwa kioo ndani ya Muungano wetu. Mhe. Mwenyekiti, muungano bado naendelea kusema ni dhahabu na dhahabu hii inatunzwa na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Wazanzibar wote kwani Muungano umeleta tija kubwa kwa Wazanzibari na nchi yao.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia nataka niseme tu kwamba hali ya mazingira ya Zanzibar ni mazingira mazuri kutokana na kusimamiwa vyema amani na utulivu ambayo sasa hivi ndio dira inayoonesha maendeleo ya Wazanzibar.

Mhe. Mwenyekiti uwo ndio mchango wangu, ahsante sana naunga mkono hoja. (*Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa mchango wako sasa naomba nimwite Naibu Waziri wa Habari.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nami kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hutuba hii ya Oofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba niungane na wenzangu nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuamsha salama na kushiriki katika Baraza lako hili tukufu kwa siku ya leo. Mhe. Mwenyekiti, vile vile naomba nimshukuru Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuniteua tena kuwa Naibu wa Habari Utalii na Mambo ya Kale (*Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nawashukuru sana wanawake wa Mkoa wa Kaskazini Pemba kwa kunichagua na kunipa ridhaa zao na kuendelea kunipa mashirikiano ya kuwakilisha katika Baraza hili Tukufu. Lakini vile vile Mhe. Mwenyekiti nichukue fursa tena kumpongeza Mhe. Rais pamoja na Mhe. Waziri, Katibu Mkuu Kiongozi na watendaji wake wote kwa mashirikiano yao mazuri ambayo wanatuongoza sisi lakini pamoja na wananchi wa Zanzibar kwa hekma na busara za hali ya juu.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, vile vile Mhe. Rais anaonesha upendo wa dhati kwa yale ambayo yote anayatekeleza na kuyafanya zikiwemo kutekeleza ahadi ambazo ameziahidi wakati wa uchaguzi na pia na kutekeleza Ilani ya CCM.

Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba niende moja kwa moja kwa upande wa vyombo vya habari. Mhe. Rais katika kipengele hiki cha vyombo vya habari ukurasa 13 kifungu cha 32 Mhe. Rais katika kipengele hiki naomba nichukue fursa tena nimpongeze kwa aina ya peke yake kwa kutekeleza malengo ya kuviboresha vyombo vyetu vya habari Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, lengo la serikali ni kuhakikisha kwamba wananchi wa Zanzibar wanapata habari kwa uhakika. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Suleiman Sarahan Said hapa kataka kwamba iweko *channel*, yaani kuwe na *free channel* za *ZBC*. Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba nimjibu Mhe. Suleiman Sarahan. Mhe. Rais anawapenda sana wananchi wake na hapa ameboresha kwa *channel* ambazo zipo kiasi ambacho amepewa hii *free* sisi ving'amuzi tunauza kwa bei ya shilingi 65,000/= kwa mwezi.

Mhe. Mwenyekiti, hii kwanza naomba nimpongeze Mhe. Rais pia ana imani na wananchi wake na kuona kwamba wananchi wanapata habari na hakuna TV yoyote kwa Tanzania hii ambayo wametoa ofa kama hii kwa ving'amuzi tunavyoviona vinauzwa katika TV zetu nyengine au vyombo vyetu vya habari ambazo wana ving'amuzi na sisi Mhe. Rais kaona ni vizuri sana na wananchi wake. Lengo la vyombo vya habari ni kuhabarisha na kuburudisha. Lakini naomba niseme kwamba uwezekano upo wa kuweka hii *channel free* ila naomba tu nimshauri sana Mhe. Sarahani ajue kwamba hili ni shirika na shirika linatakiwa lijiendeshe wenyewe. Kwa hivyo kwa hili Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Sarahani aliangalie kwa kina na angalie kwamba shirika linahitajika lijiendeshe.

Mhe. Mwenyekiti, zaidi nilikuwa nichangie kipengele hichi cha *ZBC* kwani kuna na magazeti pia nayo, magazeti yote nchini yana bei tofauti na magazeti yetu ya Zanzibar. Magazeti yetu ya Zanzibar pamoja na gharama za uchapishaji lakini sisi tunauza gazeti kwa shilingi 500/= kwa

kila mwananchi ili tunahakikisha kwamba wananchi wetu wanapata habari ambayo au ambavyo hawana gharama kubwa ya kupata gazeti hili lakini na kuchangia kwa upande wa vyombo vya habari, kwa upande wa matangazo ya redio na mengineyo.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho kabisa naomba niunge mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja na pia niwashauri Waheshimiwa wenzangu kwamba tuwapitishie bajeti yao hii Ofisi hii ya Mhe. Rais ili tuone kwamba yanatekelezwa. Mhe. Rais anaendelea kutekeleza yale mazuri ambayo yamo katika hotuba hii.

Ahsante Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana nakushukuru Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale, sasa waheshimiwa wajumbe naomba nimwite Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ili atowe majumuisho kwa zile hoja zilizotolewa na wajumbe.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uzima na afya njema lakini pili sina budi kukushukuru wewe Mhe. Mwenyekiti kwa kuweza kunipa nafasi ili tuweze kutimiza wajibu wetu wa kufanya majumuisho kama ilivyo desturi baada ya kupokea michango, maoni na ushauri unaotoka kwa waheshimiwa wajumbe.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nichukuwe nafasi hii kwa mara nyengine tena, naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa kunipatia fursa hii kwa kuweza kufanya majumuisho yanayotokana maoni, mapendekezo kuhusiana na suala zima la bajeti la Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa Mwaka huu wa fedha 2018/2019.

Mhe. Mwenyekiti, shukrani za kipekee naomba ziende kwa Mhe. Panya Ali Abdalla Mwakilishi wa Viti Maalum Wanawake Mkoa wa Kaskazini Unguja ambaye aliwasilisha Hotuba kwa niaba ya maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu na akimuwakilisha Mwenyekiti wake Mhe.Omar Seif Abeid, Mwakilishi wa wananchi Jimbo la Konde.

Mhe. Mwenyekiti, niwashukuru Wajumbe wote wa Kamati hii wameweza kutupa ushirikiano na kufanya kazi nao kwa pamoja na ninawaomba niwaahidi na niwasibitishie kwamba ushuirikiano wao na ushirikiano wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi hauna mbadala tutajitahidi kufanya nao kazi kwa pamoja ili tuweze kufikia malengo na madhumuni ya kuwepo kwa ofisi lakini pia kuwepo kwa kamati hizi za kudumu.

Mhe. Mwenyekiti, jumla ya Waheshimiwa Wajumbe ishirini na saba wameweza kuchangia Bajeti ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Wajumbe ishirini wakichangiza kwa njia ya kawaida kwa maana kwamba kwa kupata fursa ya kusema na wakumbe saba wameweza kuchzangia kwa njia ya maandishi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nichukuwe nafahi hii kwa kuwataja kwa majina:

1. Mhe. Panya Ali Abdalla
2. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)
3. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy
4. Mhe. Machano Othman Said
5. Mhe. Suleiman Makame Ali
6. Mhe. Ali Khamis Bakari (Doholo)
7. Mhe. Simai Mohammed Said (Mpakabasi)
8. Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil
9. Mhe. Rashid Makame Shamsi
10. Mhe. Hamza Hassan Juma
11. Mhe. Shaib Said Ali
12. Mhe. Suleiman Sarahan Said
13. Mhe. Juma Ali Khatib
14. Mhe. Mohamed Said Mohamed (Dimwa)
15. Mhe. Bahati Khamis Kombo
16. Mhe. Shehe Hamad Mattar
17. Mhe. Miraji Khamis Mussa (Kwaza)
18. Mhe. Jaku Hashim Ayoub
19. Mhe. Maryam Thani Juma
20. Mhe. Said Soud Said
21. Mhe. Chum Kombo Khamis

Kwa upande waliochangia kwa maandishi:

1. Mhe. Abdalla Maulid Diwani
2. Mhe. Bahati Khamis Kombo
3. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed
4. Mhe. Zaina Abdalla Salum
5. Mhe. Mohamed Mgaza Jecha
6. Mhe. Hamida Abdalla Issa
7. Mhe. Ussi Yahya Haji

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kuwatambua wachangiaji hao sasa naomba nichukuwe nafasi hii kutoa ufafanuzi wa baadhi ya hoja ambazo zimeulizwa na waheshimiwa wajumbe.

Kiujumla michango ilikuwa karibu sehemu sita ambapo wachangiaji wengi walichangia zaidi katika kutowa pongezi, wa pili walichangia katika utekelezaji na ufuatiliaji wa ahadi za Mhe. Rais, sehemu ya tatu zilizokuwa zinafanana ni suala la ziara zinazofanywa na Mhe. Rais ndani na nje ya nchi, sehemu ya nne ilikuwa inahusina na masuala ya *DIASPORA*, sehemu ya tano ilikuwa inahusiana na masuala ya ushirikiano wa kikanda na sehemu ya sita ilikuwa masuala zima ya kuimarisha mawasiliano yaani Kurugenzi ya Mawasiliano Ikulu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kulihakikishia Baraza lako tukufu kwamba pongezi na salamu walizozitoa kwake waheshimiwa wajumbe kwa ajili ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, nawathibitishia kwamba salamu hizi nitazifikisha. Na tutazifikisha kwa

uzito ule ule kama zilivyozitoa hata hivyo, kwa kuwa Mhe.Rais ni mfuatiliaji mzuri wa shughuli za Baraza hili, naamini atakuwa tayari yeye mwenyewe ameanza kuzisikia. Naomba Waheshimiwa Wajumbe, na mimi nakubaliana nanyi kwamba Mhe.Rais amefanya kazi kubwa nzuri ya kupigiwa mfano na ndio maana kwenye kitabu chetu tukasema tumuunge mkono Mhe. Rais kwani amefanya kazi iliyotukuka. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naomba niendelee kwa kuchukua nafasi ya kutoa ufafanuzi kwa baadhi ya hoja ambazo zinatokana na taarifa ile ya kamati.

Mhe. Mwenyekiti, ukitazama tija na faida ambayo imepatikana kutokana na ziara hizi kwa kuanzia na ziara ya Mhe. Rais katika Umoja wa Falme za Nchi ya Kiarabu (UAE), ni faida kubwa yenye tija na maslahi makubwa kwa upande wa Zanzibar na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwanza ni kudumisha na kuendeleza uhusiano wetu wa kidiplomasia lakini pili ni fursa ziliopo kama ambavyo tumeleza kwenye kitabu chetu lakini pia katika jarida maalumu ambalo tumelitowa kuhusiana na ziara hii ni imani yetu kwamba yale yote mazuri tutakuwa tumeyafatilia na tutayafatilia na tutayasimamia ili yaweze kutekelezeka, na katika hili kama vile ambavyo Mhe.Mohamed Said Mohamed (Dimwa) ameuliza serikali imeunda Kamati Maalum kwa ajili ya kufuatilia na kuhakikisha kwamba yale tuliokubaliana yanatekelezwa kwa vitendo na wananchi wetu wanaona. Kwa hiyo kuna kamati maalum ambayo serikali imeunda inaratibu na kufuatilia na imani yangu kwamba yote sekta ambazo zitakuwa zinahusika itachukua hatua katika kuona mambo haya yanakwenda kwa *materialize* ili tija iliyokusudiwa iweze kuonekana.

Mhe. Mwenyekiti, jengine kubwa lilikuwa ni ushauri unaohusiana na masuala ya uimarisha wa huduma za mawasiliano niwathibitishie kwamba suala la mawasiliano na kuweka karibu baina ya serikali na wananchi wao, kuweza kupata taarifa ya yote yanayotendeka katika serikali hili tumelichukua na tutazidi kulichukulia hatua kuweza kuona kila mwananchi alipo awe ndani ya Zanzibar ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ulimwengu mzima kwa ujumla kwa kupitia njia za kisasa zilioko za vyombo vya habari tutahakikisha kwamba taarifa na habari hizo zinawafikia watu wote ulimwenguni kuweza mazuri yanayotendwa na Mhe. Rais.

Mhe. Mwenyekiti, jengine lilikuwa linahusiana na suala la kuongeza jitihada katika kuwavutia wawekezaji wanaokuja nchini kuondoa usumbufu na bugudha na mategemeo yetu kwamba taasisi na sekta husika wanatakuwa wana wajibu wa kufanya hilo kwa sote tunajua nchi yetu ni nchi ambayo inategeme uchumi wa huduma na ili uweze kuwa na uchumi mzuri wa huduma maana yake unatakiwa uwe na mfumo mzuri zaidi wa kukaribisha watowaji wa huduma na wawekezaji waweze kuchukua muda mfupi kuweza kupata vibali na ruhusa ya kuweza kuwekeza. lakini pia tuweze kuwalinda kwa masharti ya nafuu lakini pia kuwapa *incentives* ambazo zitaweza kuwavutiza waje kuzekeza kwako na wasiende kuwekeza nchi nyengine. Kwa hiyo mategemea yetu kama kuna kasoro katika suala zima la uvutiaji na uwekezaji tutahakikisha kwamba serikali itafanya serikali itafanya jitihada za ziada kuweza kuwalinda na kuweza kuwashajihisha na kuwavutia wawekezaji waje vizuri zaidi na waweze kupata nafasi ya kuwekeza kwa muda zaidi kama ilivyo malengo ya serikali.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa Pemba, nazipokea pongezi zote zilizotolewa na Afisa Mdhamini Ndugu Amour Hamad Saleh kwa utendaji na usimamizi mzuri wa Ofisi ya Rais na

Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Pemba matumaini yetu kwamba mtendaji wetu huyu hatokuwa yule mgema wa tembo kwa maana amesifiwa atalitia maji, imani yetu kwamba ataendelea kubali hapo hapo alipo katika utendaji wake na atajipa jitihada ya kuweza kuisharisha na kuboresha utendaji wa kazi zake.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine liloulizwa lilikuwa ni suala la Mhe. Nadir alilouliza masuala mazima yanayohusiana na masuala ya *DIASPORA*, juu ya hatua gani ambazo serikali ambazo tunaweza kuzichukua katika kuimarisha, kuwasaidia. Naomba nimthibitishie tu Mhe. Nadir kwamba katika sera yetu ile ni kuonesha dhamira ya serikali katika kwenda katika utungaji wa sheria...

Mhe. Mwenyekiti: Kuhusu utaratibu Mhe. Mohamed Said Mohamed

UTARATIBU

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Mwenyekiti nilikuwa nikiomba muongozo wako Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza anajumulisha na kuweza kupata lakini ajabu yangu ninayoiona mbele kote hakuna Mawaziri sasa sifahamu tunaweza tunaijumuisha hii kama waheshimiwa hawana nafasi basi ningeomba Baraza lako hili tuweze kuliahirisha mpaka jioni ili Mhe. Waziri aje kujumuisha na mawaziri wakiwa wametangulia mbele. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, hii tunayoipitisha hapa ni bajeti ya Mhe. Rais na mawaziri unaona kama ilivyo hakuna sasa ningeomba muongozo wako juu ya hilo.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Mhe. Mohamed Said Mohamed (Dimwa) umetaka muongozo kuhusu suala hilo basi mimi naomba mheshimiwa aendelee lakini niiombe serikali waitane wawepo na kabla hatujapitisha vifungu basi nitalazimika kuahirisha Baraza kama mawaziri mbele hawatakuwepo. *(Makofi)*

Kwa hiyo naomba sana na nina imani wapo kwa sababu labda wameenda kunywa chai na mabo mengine lakini naiomba sana Mawaziri wawepo kabla hatujapitisha hivyo vifungu.

Ahsante Mheshimiwa.

Mhe. Machano Othman Said: Mhe.Mwenyekiti kuhusu utaratibu Kanuni yetu ya Baraza haituzuwii kupitisha bajeti yetu ya Ofisi ya Rais kama Mawaziri hawapo ingawa mawaziri wana utaratibu wao wa kuwajibika kwa pamoja lakini kanuni zinaturuhusu hata kama hawakuja tuendelee na tupitishe vifungu kama ilivyo kawaida.

Mhe. Mwenyekiti: Nakushukuru Mheshimiwa lakini nimetoa ufanunuzi kuwa itapendeza zaidi na wao wawepo ijapo kuwa kanuni zetu zinaruhusu hivyo, lakini nina imani Mawaziri wengine wapo na serikali ipo na mawaziri pia wapo basi tuendelee naomba tuendelee mheshimiwa.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, naomba nimshukuru Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf kwa mchango wake ambao

ameutowa kuhusiana na suala zima la *DIASPORA* kwa kiasi gani ambayo tutaweza kuwasaidia *DIASPORA* katika masuala ya kuweze kuwatambua lakini pili michango yao na *incentives* gani ambazo tutawapatia.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sheria ya Ukaazi ya Usajili wa Zanzibar suala la kutambua kuwapa vitambulisho si suala gumu ni suala ambalo tutakamilisha taratibu zetu na tunaamini kwamba itakuwa vyema na busara kwa *DIASPORA* hawa kuweza kuwatambua na kuwapa vitambulisho maalumu ambavyo vitakuwa vinawapa tija na faraja ya wao kuweza kutambulika. Lakini pili tuweze kutazama utaratibu mzima wa kuweza kuwasaidia katika utozwaji watozo katika masuala ya *VISA* lakini pia fursa ambazo wataweza kuzipata wao sasa kama wao wenyewe watakuja kuwekeza au watakuwa wao wabia au washirika wa wawekezaji ambao watakuja nao hapa nchini, kiujumla sera ya *DIASPORA* inamakusudia ya kuweza kumsaidia *DIASPORA* kuweza kunufaika vizuri zaidi na sheria zilizopo nchini.

Linalohusiana na masuala ya ulinzi na usalama nimthibitishie kwamba majengo yetu yote yako salama na vyombo husika vinaendelea kuchukua jitihada na juhudi za kuweza kufanya nguvu katika kuimarisha utoaji wa usalama katika nyumba zetu zote za Ikulu.

Mhe. Mwenyekiti, tumepokea pongezi za Mhe. Machano Othman Said na tunamshukuru sana kwa mchango wake ambao umejaa uweledi na falsafa ya diplomasia na ushirikiano wa kimataifa. Mheshimiwa Machano ametutaka kutuhakikisha kwamba Zanzibar inashiriki vizuri katika mikutano ya ngazi zote za Jumuiya za Mtangamano wa Kikanda. Vile vile, suala hili limezungumzwa na Mhe. Hamza Hassan Juma, Mhe. Mohamed Said Mohamed (Dimwa) na wao pia wameona kwamba upo umuhimu wa kurugenzi yetu na serikali kwa ujumla kuweza kushiriki, niwathibitishie tu kwamba Ofisi ya Rais kuwa *co-ordinator* tutajitahidi kufanya uratibu mzuri wa kuweza kuona kwamba serikali kwa taasisi zake zote zinaweza kushiriki katika vikao vyote vya kikanda ili kukidhi matakwa haya ya kwenda katika metengemano.

Lakini pili kuweza kufahamu maamuzi yanayotokana na vikao hivi vya Ushirikiano baina ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na nchi nyengine katika mashirikiano ya kikanda yakiwa Jumuiya ya Afrika Mashariki yakiwa ya *SADC* na yakiwa mengine yoyote yale.

Mhe. Mwenyekiti, tumepokea salamu za Mhe. Suleima Makame Ali kwa mchango mzuri na tunamthibirisha kwamba suala la *DIASPORA* nalo litakuwa pia tumelingatia vizuri na tutahakikisha kwamba *DIASPORA* wanaweza kunufaika kwa namna moja au nyengine kutokana na utayarishaji na uharakishaji wa sheria zitakazoundwa hapo baadae.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusiana na suala na pili kwa la tatu la ahadi za Mhe. Rais katika sekta mbali mbali niwathibitishie Mhe. Mwenyekiti kwamba wajibu wa ofisi yetu ni kuzikumbusha taasisi na sekta husika kuona kwamba yale yote ambayo Mhe. Rais ameyaahidi, basi ni wajibu wa serikali kuweza kuona kuyatekeleza na katika utekelezaji bila shaka kutakuwa kuna mipango ya sekta husika katika kupanga mfumo na utaratibu mzuri ili kuweza kutekeleza ahadi zetu hizi. Ni imani yetu kwamba taasisi zote za serikali tutaendelea kuwahimiza na kuwakumbusha ili kuweza kufanikisha mambo yote ambayo yatakuwa Mhe. Rais ameweza kuyaahidi katika sekta zote husika.

Mhe. Mwenyekiti, katika hili nataka niongezee na lile la Mhe. Hamza Hassan Juma alitaka kujua suala zima la ahadi ya Mhe. Rais katika ujenzi wa barabara iliyotoka Shaurimoyo mpaka Darajabovu kupitia Mboriborini. Nimthibitishie tu Mhe. Hamza kwamba tayari sekta husika jambo hili wanalo wameshatenga fedha na imani yangu kwamba watakapokuja kuwasilisha bajeti yao, jambo hili watatoa ufafanuzi mzuri katika maelezo ambayo Mhe. Waziri ataweza kuyatoa.

Pili, katika hili la Mhe. Hamza Hassan Juma alitaka kujua suala zima la msitu wa Ngezi nimthibitishie tu kwa kutumia nafasi yake kama mwakilishi lakini pia kama mwenyekiti. Imani yangu ni kwamba sekta husika ya Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati watakapokuja watakuwa na maelezo mazuri sana yanayohusiana na suala hili la msitu wa Ngezi namna ya kuweza kugawanya msitu, lakini pia na eneo la wananchi kwa ajili ya kutumia huduma zao kama vile ambavyo serikali ilikuwa imeahidi.

Mhe. Mwenyekiti, pia nimepokea mchango wa Mhe. Shaib Said Ali ameomba kutoa hofu kuhusiana na masuala ya fedha zilizopangwa 2018-2019. Ni kwamba kwa mujibu wa mahitaji vipaumbele vyetu fedha hizi tunaamini kwamba zitaweza kutusaidia sana na zitaweza kukidhi yale matakwa ambayo tumekuwa tumeyalenga katika kipindi hiki.

Mhe. Mwenyekiti, utaratibu wa serikali kwamba mnapanga utaratibu kuna miradi ambayo mnakamilisha katika mwaka mmoja, ipo miradi ambayo mnakamilisha katika miaka miwili na ipo miradi ambayo mnakamilisha katika kipindi cha miaka mitano. Kwa hiyo, fedha hizi nyingi tutatekeleza katika ile miradi ambayo tutakamilisha mwaka huu, lakini kwa ile miradi ambayo itakuwa inaendelea basi fedha hizi zitakuwa zimeanza na mwakani tutaweza kuongeza fedha katika kukamilisha jambo zima ambalo litakuwa linahusiana na ukamilishaji wa miradi hii.

Mhe. Mwenyekiti, wachangiaji wengine ambao wamekuja kuchangia mwisho hapa alikuwa ni Mhe. Maryam Thani Juma ameulizia kwa kina kirefu suala zima la ahadi ya Mhe. Rais katika suala zima la ulipaji wa fidia. Nimthibitishie tu kwamba sisi ofisi yetu tutaendelea kuratibu kwa sekta husika ili kuweza kuona na wao wanatimiza wajibu wao kama ambavyo Mhe. Rais ameshaahidi kuona kwamba hakuna mwananchi ambaye nyumba yake itavunjwa bila ya kulipwa fidia katika ujenzi wa barabara na kama kuna mtu ambaye itakuwa nyumba yake imevunjwa basi huo ni utaratibu wa kiserikali na ahadi ya serikali kwamba mwananchi huyo atalipwa fidia yake kama ambavyo ameweza kuahidiwa.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mohamed Said Mohamed ukiachilia mbali yale mengi ambayo ameyasema ya *page to page*, ambayo kwa hapa nitamuomba baadae tutatoa ufafanuzi mzuri zaidi katika vifungu, kwa sababu hatuwezi kusoma *page* kwa *page* kwa hapa tulipo. Lakini nimuhakikishie lile suala moja kubwa ambalo amelisema linalohusiana na kitabu chetu, kwamba Mhe. Rais alipokwenda ziara katika kitabu tumeandika kwamba 2011 kulikuwa kuna *MOU*. Suala la Mhe. Mohamed Said Mohamed kwamba kwa nini tusiingie mkataba na badala yake tumeingia *MOU*.

Mhe. Mwenyekiti, *MOU* si tu kwa lugha ile ambayo umeitumia, kwamba ni makubaliana na ki-*gentlemen* hapana. *MOU* ni msingi mzuri wa kuanza kufikia katika mikataba mikubwa ya

kimataifa. Mnapoanza kwenye *MOU* maana yake mnaanza kujenga uelewa wa pamoja, mnapata fursa ya kuzungumza kwa pamoja kama kuna kasoro mnajadili kwa pamoja ili mkifika pahali pakufika kwenye makubaliano mnakubaliana kwa pamoja. Kwa hiyo, *MOU* hii ndio ambayo imetujenga uhusiano wetu sisi na Ras al-Khaimah na tayari kwa kujenga mawasiliano yetu mazuri tumeweza kupata manufaa ikiwemo uchimbaji wa visima wanaendelea na mazoezi. Lakini kubwa zaidi kama serikali ingeweza kutaka kuingia mkataba maana yake tungeingia mkataba kwa utaratibu gani chini ya suala hili la mafuta.

Sote tunajua kwamba kipindi cha 2011 suala hili la mafuta bado lilikuwa lina mvutano baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Zanzibar. Na baada mwaka 2014 ndio Serikali ya Jamhuri ya Muungano wakatunga sheria ambayo waliondoa suala hili katika mambo ambayo yangekuwa yanasimama moja kwa moja na sheria ya Jamhuri. Na mwaka 2016 Serikali ya Zanzibar ndio tumetunga sheria, sheria Nam.6 ambayo inatuwezesha sasa kuweza kuingia mikataba yanayohusiana na mambo ya mafuta bila ya kuwa na mgogoro na mvutano na taasisi nyengine yoyote. Kwa hiyo, imani yangu kwamba ni busara kubwa kuingia *MOU* mwanzo mnafanya majadiliano baadae mnapokubaliana vizuri mnakwenda katika mikataba mikubwa yakuweza kujifunga.

Mhe. Mwenyekiti, pia Mhe. Mohamed Said Mohamed alizungumzia suala la ukurasa wa 17 na kuwaomba kwamba taasisi nyengine ziweze kufata utaratibu huu mzima. Naamini mawaziri watakuwa wamekusikia na aliulizia suala la kamati kama imeundwa kufatilia suala la ziara. Nimthibitishie tu kwamba kamati imeundwa na inafanya kazi vizuri na inatoa taarifa zake serikalini katika kipindi kipindi cha mwezi kamati hii inatoa taarifa serikali katika ufatiliaji mzuri wa taasisi hii. Pia ziara hii imezaa matunda mengi kama vile ambavyo tumesema, imani yetu kwamba kila muda unapokwenda serikali itaendelea kutoa taarifa kwa wananchi wao kutokana na matunda na faida kubwa inayotokana na ziara hii ya Mhe. Rais katika nchi za Falme za Kiarabu.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo amelisema Mhe. Mohamed Said Mohamed ni suala la ukurasa wa 47, suala zima la mafao ya wastaafu viongozi na amegusia suala la Mhe. Spika mstaafu. Nimthibitishie tu kwamba serikali jambo hili tumeliona, tumelizingatia na hatua stahiki tutazichukua.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Bahati Khamis Kombo kubwa zaidi ametoa pongezi juu ya utekelezaji wa Mhe. Rais katika masuala ya elimu, afya, miundombinu na mengineyo na ameiomba serikali kwamba tuendele kuchukua jitihada. Tunamuahidi kwamba tutachukua jitihada hizo.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Shehe Hamad Mattar ametaja kujua kuna ufanisi gani ambao utakuwa umepatikana baada ya kuongeza mshahara. Imani yetu kwamba serikali inaongeza mishahara ikiwa ni sehemu moja ya kumjenga *moral* mfanyakazi wake. Kwa hiyo, mategemeo makubwa ya serikali baada ya kuongeza nyongeza hii ya mishahara wafanyakazi watapata muda mzuri wa kuweza kukaa kazini, kuweza kujikita fikra na mawazo yao katika masuala ya kazi lakini pia kujipa muda mzuri zaidi wa kuweza kuwajibika. Na kipimo chetu kwamba kama haitakuwa hivyo maana yake serikali itaendelea kutafuta njia nyengine nzuri zaidi ya kuweza kuwahimiza

wafanyakazi ili kuweza kutoa huduma nzuri zaidi na kuweza kufikia yale malengo yaliopo ya serikali ya kuweza kurahisisha huduma kwa upatikanaji wake kwa wananchi wetu.

Mhe. Miraji Khamis Mussa alitaka kujua suala la uzinduzi wa sera ya *DIASPORA*. Ni kweli sera hii tumeizundua tarehe 09/05/2018 saa 7:40 katika ukumbi wa Baraza la Wawakilishi la zamani.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ambalo alitaka kujua Mhe. Miraji Khamis Mussa ni kama je tuna *database* ya *Diaspora*. Mpaka sasa hivi hatuna *database* ya moja kwa moja, na hatuna *database* kwa sababu *Diaspora* yenyewe wamekuwa wako maeneo mbali mbali. Lakini utaratibu na malengo yetu kwa kupitia vyama vyao tunaamini kwamba kila nchi *Diaspora* wakiwa na chama chao kwa kupitia Balozi zetu na kwa kufanya kazi ambazo zinafanywa *coordination* na idara yetu, tunaamini kwamba si muda mrefu tutakuwa tuna *database* kamili ya *Diaspora* wote walioko duniani. Tunatambua ugumu wa jambo lenyewe, changamoto ziliopo kutokana na sababu na mazingira waliyoondokea watu wetu, lakini wale ambao watakuwa wako tayari kujisajili tutahakikisha kwamba tunaipata *database* hiyo na tunaitumia vizuri kama malengo ya sera na sheria ya *Diaspora* itakapokuja baadae katika kurahisisha na kushajihisha maendeleo kwa faida ya wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, jengine analotaka kujua Mhe. Miraji Khamis Mussa ni suala la faida ya wafanyabiashara wetu katika Soko la Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mhe. Mwenyekiti, faida kubwa ya soko ni kama ilivyo soko jengine ukiwa na utaratibu mzuri wa kutengeneza bidhaa nzuri, ukiwa umepata wigo mpana wa kuwa na soko maana yake ni fursa kwa mfanyabiashara kuandaa bidhaa zake nzuri kuingiza kwenye soko. Umuhimu wa soko ni kwamba soko linapokuwa kubwa maana kunakuwa na utayari wa ununuzi unakuwa ni mkubwa zaidi. Kwa hiyo, imani yetu kwamba wafanyabiashara wetu watakuwa wamepata fursa pana zaidi ya kuwa na soko la takriban nchi sita sasa bila ya kuwa vikwazo kwa mujibu wa sheria na taratibu husika za kila nchi chini ya usimamizi na mwamvuli wa mtengamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mhe. Mwenyekiti, pia alitaka kujua habari ya Kamati ya Kufatilia, tayari nimeshalitoa ufafanuzi kwamba tayari kamati imeshaundwa.

Mhe. Mwenyekiti, mchangiaji aliyefuata alikuwa ni Mhe. Jaku Hashim Ayoub. Sehemu kubwa Mhe. Jaku alichukua nafasi ya kumsifu na kumshukuru Mhe. Rais kwa namna ya kipekee anavyosimamia kazi na uwajibikaji wa shughuli mbali mbali za serikali na namna ambavyo Mhe. Rais ameweza kusimamia utekelezaji mzuri wa ilani ya Chama cha Mapinduzi katika sekta na huduma zote ikiwemo afya, elimu na mengineyo. Ni imani yetu kwamba Mhe. Rais yeye akiwa kiongozi wetu mkuu ni wajibu wetu mawaziri na watendaji wa serikali kufuata na kuyatekeleza yale yote ambayo Mhe. Rais atakuwa ametuelekeza. Na nikuahidi Mhe. Jaku kwamba wajibu wetu sisi kama serikali tutafanya kwa jitihada zetu zote kuhakikisha kwamba yale ambayo yameahidiwa katika ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi tunayatekeleza kwa vitendo.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho zilikuwa ni pongezi kwa ujumla. Kwa ujumla naomba nichukue nafasi hii kuwashukuru wachangiaji wote walioweza kuchangia kwa namna moja au nyengine na

kama kutakuwa kuna mtu sikumtaja basi nitakuwa nimekosea kama binadamu, lakini si madhumuni yangu yakutokutambua mchango wake. Lakini suala la Mhe. Mohamed Said Mohamed ambalo ameulizia suala la vifungu chini ya kurasa wa 1 - 6 wa bajeti labda inawezekana ikawa jadweli lina makosa ya kiuchapaji, lakini kama kuna haja ya kutoa ufafanuzi zaidi Mhe. Mwenyekiti, tukiahidi kwamba tutamsaidia Mhe. Mohamed Said Mohamed kuweza kupata.

Mhe. Mwenyekiti, malengo tuliyoyakusudia na taarifa zetu ni kuona kwamba mambo haya yanakwenda vizuri, na kama kuna kasoro yoyote ukiachilimbia mbali tena ubinadamu basi tutakuwa tuko tayari kutoa ufafanuzi kila pahali ambapo Waheshimiwa Wajumbe watahitaji ufafanuzi huo sisi tutakuwa tayari kutoa ufafanuzi.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache mimi mwenyewe binafsi naomba nichukue nafasi hii kwa niaba ya wananchi wenzangu wa Jimbo la Chwaka kukushukuru wewe, kumshukuru Mhe. Rais lakini pia kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote kwa namna ya kipekee walivyoweza kuchangia kutushauri, kutuelekeza na mimi niwaahidi yale yote mazuri ambayo mmetuahidi kutushauri na kuchangia tunaahidi kwamba sisi tutayachukua na kwenda kuyafanyia kazi. Na pale panapo mapungufu msisite muendelee kutuhimiza tuchukue jitihada ya ziada kuona kwamba tunaongeza ufanisi kwa kuimarisha malengo na maslahi ya Mzanzibari.

Tatu Mhe. Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kwa niaba ya wananchi wenzangu wa Jimbo la Chwaka kuiunga mkono hotuba ya bajeti hii ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ya 2018-2019. Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, hoja imetolewa sasa naomba niwahoji wanaokubaliana na hoja hiyo, wanaokataa, wanaokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Kabla sijamwita Mhe. Waziri naomba nimwite Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ili atengue Kanuni ya muda tupate tumalize shughuli zetu kwa leo.

KUONGEZA MUDA WA BARAZA

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, naomba tuweke kando Kanuni ya muda kifungu 23(1) ili tuweze kumaliza shughuli zilizo mbele yetu na kutoa nafasi kwa Waheshimiwa Wajumbe jioni hii kupumzika. Kwa hiyo, naomba tuweke kando Kanuni ya muda mheshimiwa naomba kutoa hoja. Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Nakushukuru Mhe. Waziri, Waheshimiwa Wajumbe hoja imetolewa sasa naomba niwahoji wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Baraza lako limejadili na kuikubali hotuba ya bajeti ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili kuvipitisha vifungu vya matumizi vya Wizara ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

KAMATI YA MATUMIZI

FUNGU A01 – OFISI YA RAIS NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI

Kifungu PA0101	-	Programu Kuu ya Kusimamia Huduma na Shughuli za Mhe. Rais na Kuimarisha Mawasiliano Ikulu	
Kifungu SA010101	-	Programu Ndogo ya Kusimamia Huduma na Shughuli za Mhe. Rais	4,557,865,000
Kifungu SA010102	-	Programu ndogo ya Kuimarisha Mawasiliano baina ya serikali na wananchi	

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Mwenyekiti, Katibu alisoma sivyo kasoma kifungu kikubwa wakati kuna vifungu vidogo vidogo sijui tunakwendaje hapa, kwa sababu hakwenda vizuri.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe Katibu amesoma hivyo amesema ameanza kusoma hii programu ndogo halafu atakuja kuisoma ya pamoja. Lakini pia anakwenda kutokana na *volume* za hizi.

Tuendelee Katibu

Kifungu PA0101	-	Programu Kuu ya Kusimamia Huduma na Shughuli za Mhe. Rais na Kuimarisha Mawasiliano Ikulu	4,998,724,000

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Mwenyekiti, hapa katika mchango wangu nilisema hawa mwaka jana walipewa shilingi 306,389,000/- lakini mara hii wamepewa shilingi 359,950,000/- na kutokana na majukumu mengi ambayo wanafanya nilisema nina nia ya kukikamata kifungu, ili kifungu hiki kiongezewe kutokana na umahiri na kazi ambazo wanazifanya.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri tuko pamoja kwanza?

Sasa tulirejea kifungu kile kile cha kwanza ambacho alikisoma Katibu na Mhe. Mjumbe akasema kuwa tunakwenda vipi na tukampa taratibu. Kwa hivyo kimeanza kile cha mwanzo tumesoma programu kuu. Mhe. Mohamed Said Mohamed rejea hoja yako tena ili Mhe. Waziri asikie.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mheshimiwa kwenye kifungu kidogo cha SA010201 kuratibu shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Kikanda na Kitaifa.

Nilipokuwa nikichangia nilizungumza kuwa mwaka jana wamewekewa shilingi 306,389,000; mara hii wamewekewa shilingi 359,950,000. Nikazungumza kuwa kazi inayofanywa hapa ni kubwa sana, kwa hivyo kuna baadhi ya vifungu tutaviondoa. Sasa nilikuwa naomba maelezo.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe tulikuwa hatujafika tulianza mwanzo kwa mujibu wa hoja yako uliyoitoa. Kwa hivyo tunaanza hiki halafu tunafuata hiyo programu unayosema.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Mwenyekiti, basi ninayo hoja hapo hapo juu kwenye kifungu...

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa naomba ukae.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Sasa tunakwenda *vice versa* hatuwezi tutapitisha vipi. Mhe. Mwenyekiti, unatuendesha vibaya, wengine tutakuwa hatuwezi kuhoji.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mohamed Said Mohamed tumeanza na kifungu kile ambacho ulichosema cha pili bado hakijafika, sasa sijui tunaendesha vibaya vipi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe kifungu kimekubaliwa.

Wajumbe: Ndio.

Kifungu PA 0102	-	Programu Kuu ya Kuratibu Ushirikiano wa Kikanda, Mashirika ya Kimataifa na Wazanzibari wanaoishi Nje ya Nchi.	537,965,000
Kifungu PA 0103	-	Programu Kuu ya Utawala na Uendeshaji wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi	2,935,411,000
		Jumla Kuu ya Fungu A01	**8,472,100,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU A02 - OFISI YA RAIS BARAZA LA MAPINDUZI

Kifungu PA 0201	-	Programu Kuu ya Usimamizi wa Majukumu ya Kikatiba na Kisheria ya Baraza la Mapinduzi	509,800,000

Kifungu PA 0202	-	Programu Kuu ya Utumishi na Uendeshaji wa Ofisi ya Rais Baraza la Mapinduzi	1,451,800,000
		Jumla Kuu ya Fungu A02	**1,961,600,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

(Baraza lilirudia)

Mhe. Mwenyekiti: Tukae Waheshimiwa Wajumbe. Sasa naomba nimwite Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha Makadirio ya Fedha ya Wizara ya Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi bila ya mabadiliko sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako liyakubali makadirio haya.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.(*Makofi*)

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Waheshimiwa Wajumbe hoja imetolewa naomba niwahoji. Wanaokubaliana na hoja hiyo, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Waheshimiwa Wajumbe na mimi nichukue fursa hii kuwashukuru wachangiaji wote, lakini pia nimshukuru Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, lakini shukurani za pekee ziende kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe kabla ya kuakhirisha nilikuwa nina tangazo kutoka kwa Mwenyekiti wa UWAWAZA, wale wote wanachama wa UWAWAZA wabakie humu. Kwa hivyo Waheshimiwa Wajumbe naomba kuakhirisha hadi saa 11:00 jioni.

KUONGEZWA MUDA WA BARAZA

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, tuliongeza muda kwa dhamira ya kumaliza shughuli zetu za leo na moja katika shughuli zetu za leo lilikuwepo suala la Hotuba ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, ili tuweze kumaliza hivi sasa na jioni Waheshimiwa Wajumbe wapate nafasi ya kupumzika.

Mhe. Mwenyekiti, kama tulivyotoa hoja naomba tuendelee na utaratibu huo ahsante sana.

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Mwenyekiti, nilitaka kuungana na Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwamba leo tukimaliza shughuli ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utawala Bora, *order paper* imemalizikia hapo. Kwa hivyo ina maana jioni tunapumzika, tunakuja kesho kwa mujibu wa *order paper* hakuna kazi ya jioni.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais mwanzo tulipotengua Kanuni mimi nilijua kwa shughuli hii ambayo tumeipanga hivi sasa. Kwa hivyo kwa vile bado tutakuwepo naomba tuakhirishe mpaka jioni ili tuijadili.

Waheshimiwa Wajumbe naomba tuahirishe kikao mpaka saa 11:00 jioni.

(Saa 6:50 mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11: 00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe kama mtakumbuka kwamba tulikuwa katika *order paper* yetu ya leo tulikuwa na Hati ambayo imewasilishwa mezani inayohusiana na Hotuba ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambayo hotuba hiyo vile vile iliambatana na Hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali.

Ni ukweli kwamba serikali imeweza kutimiza masharti ya kikatiba ya kuleta hotuba hiyo. Lakini niseme tu kwamba kwa kuwa kamati yenyewe bado imeshindwa kuipitia vizuri ile Hotuba ya Serikali inayotoka kwa Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali tumejadiliana sana uongozi wa Baraza la Wawakilishi na tumeona basi, kamati ipewe nafasi ya kuweza kuipitia vizuri hotuba ile ili na wao waweze kuleta maoni yao ndani ya Baraza la Wawakilishi. Kwa maana hiyo leo hatutoweza kusoma hotuba hiyo yaani Mhe. Waziri hatosoma lakini vile vile pamoja na Mwenyekiti hatoweza kusoma hotuba hiyo.

Kwa hiyo, Mhe. Spika, ameafiki suala hilo kwa maana hiyo nitaakhirisha kikao hadi kesho saa 3:00 asubuhi. (*Makofi*)

UTARATIBU

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kuhusu utararibu Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Nimeshaakhirisha kikao Mheshimiwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: *Too much*, kwa hiyo serikali haipo. Sasa mtueleze.

(Saa 11:03 jioni Baraza liliakhirishwa mpaka tarehe 15 Mei Saa 3:00 asubuhi)